

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 11 Aprili, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Local Government Authorities for the Year ended 30th June, 2007*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUS MZEE):**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Central Government for the Year ended 30th June, 2007*).

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mashirika ya Umma na Taasisi mbalimbali kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Public Authorities and Other Bodies for the Year ended 30th June, 2007*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 41

**Mikakati ya Kukabili Tatizo la Dawa za Kulevya  
na Unywaji Gongo**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inajizatiti kukabili tatizo la dawa za kulevya nchini; na kwa kuwa tatizo hilo lina athari zinazofanana na unywaji wa pombe haramu ya gongo:-

(a) Pamoja na Serikali kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini; je, ina mikakati ipi ya kukabiliana na matumizi ya pombe haramu ya gongo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua zipi inapotokea kuwa wauzaji na wanywaji wa pombe hiyo haramu ni askari ambao ndiyo walinzi wa usalama wa wananchi?

(c) Je, Serikali inaelewa kuwa tatizo hilo ni kubwa sana huko Mkoani Manyara na linaathiri nguvu kazi ya Taifa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inayo Mikakati ya Kupambana na Tatizo la Dawa za Kulevya. Aidha, Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya iliyoundwa kwa Sheria Na. 9 ya 1995, inaratibu shughuli zote zinazofanywa na vyombo vya Dola, Idara na Asasi mbalimbali nchini, kwa lengo la kupambana na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya. Vilevile kipo kikosi kazi (*Task Force*), ambacho kinashirikisha vyombo vya dola katika kutekeleza jukumu la kukabiliana na biashara haramu ya dawa za kulevya na pia kilimo cha mirungi na bhangi, bidhaa ambazo zinazotumika kutoa dawa za kulevya na kadhalika. Kikosi hiki cha Jeshi la Polisi, sasa kinatumia vyombo na vitendea kazi vya kisasa kukabiliana pia na matatizo ya utengenezaji na matumizi ya pombe haramu ya gongo. Azma ya Serikali ni utokomezaji wa kilimo cha bhangi na mirungi, pamoja na utengenezaji na unywaji wa pombe hiyo haramu kwa njia ya operesheni za utekelezaji, sambamba na utoaji elimu kwa wananchi katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna taarifa kwamba wapo wauzaji na wanywaji pombe haramu ya gongo, ambao ni Askari wetu kule Mkoani Manyara. Askari Polisi ni walinzi wa usalama wa wananchi. Wanafanya kazi nzuri, wanashirikiana na jamii kukomesha uhalifu. Tukipata taarifa zenye shaka hiyo, suala hilo litashughulikiwa mara moja ili kuondoa tatizo hilo katika jamii. Kama ikibainika kwamba wapo askari na watendaji kama hao ni dhahiri kwamba, watumishi hao hawatusaidii na hawafai na hivyo, watachukuliwa hatua ipasavyo.

(c) Mheshimiwa Spika, tutafuatilia kwa nguvu zote ili kubaini kuwepo tatizo la uuzaji na unywaji wa gongo maeneo yoyote yale ya Mkoani Manyara na nchini kote. Hapana shaka suala zima la kupambana na kudhibiti dawa za kulevya, litatekelezwa sawia na kukabiliana na matumizi ya gongo, ambayo inaaminika ni tatizo linaloathiri nguvu kazi ya Taifa na katika jamii.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini ninaomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Baadhi ya dawa za kulevya zinaweza zikaagizwa kutoka nje ya nchi yetu na hivyo kudhibiti kwake kukawa kugumu kidogo lakini malighafi ya kutengeneza pombe haramu ya gongo inapatikana hapa hapa nchini, watengenezaji ni Watanzania wenzetu. Sasa Serikali inashindwa vipi kutoa suluhisho la kudumu la kulifutilia mbali tatizo hili la unywaji wa gongo ambalo linathiri makazi ya wananchi wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, malighafi anayoongelea ya kutengeneza gongo bila shaka ni *molasses* na *molasses* ina matumizi mengi sana. Kwa hiyo, siyo rahisi kufahamu *molasses* inayoletwa kijiji ni kwa matumizi ya mifugo, dawa au kutengenezea gongo. Kwa hiyo, ni imani yetu wale viongozi wa ngazi ya chini wanaweza kulishughulikia suala hili kikamilifu, kwa kuhakikisha kwamba, *molasses* ambayo inatumika kutengenezea gongo inapigwa marufuku katika vijiji hivyo wala isitumike kwa lishe ya mifugo yetu.

**MHE. DR. BINLITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi hii. Sasa hivi nchini mwetu tunazo pombe kali mathalani Vodigar, Wiski na Konyagi ambazo zina asilimia zaidi ya 43. Pombe aina ya gongo nayo inatengenezwa kwa utaalamu wa wananchi wetu na imekuwa ni kipato kwa baadhi ya wananchi; kwa nini Serikali isiingilie kati kuweka utaalamu unaohusika ili pombe hiyo ikitengenezwa iweze kutumika na kuingiza pato la wananchi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, yawezekana kabisa tuna pombe kali zaidi ya gongo, la msingi lililozingatwa katika kupiga marufuku pombe aina ya gongo ni kwa sababu njia inayotumika kutengenezea si ambayo inazingatia usafi na afya ya binadamu, ndiyo maana imekuwa ni haramu kwa mujibu wa sheria. Pale ambapo viwanda vya kutengeneza pombe ambayo inakubalika kwa masharti ya afya ya binadamu, vitakapoanza kutengeneza gongo, ndiyo hapo ambapo tutazingatia kuihalalisha pombe hiyo.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ninakumbuka vizuri kiwanda cha Konyagi kilipojengwa, dhumuni mojawapo ilikuwa kukusanya gongo kutoka kwa wapika gongo halafu kwenda kui-*purify* kwenye mashine na kutengeneza konyagi. Kama kumbukumbu hiyo ni sawa; je Serikali haioni kwamba badala ya kuendelea kupambana

na kitu hiki ambacho ni kigumu sana; waweke vituo mbalimbali vya kukusanya gongo ili ikatengenezwe konyagi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, hata mimi nimewahi kusikia kwamba, kiwanda cha sasa cha konyagi kilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, lengo lilikuwa ni kukusanya gongo ili ikidhi mahitaji ya afya ya binadamu. Sasa sijui hapo katikati kumetokea nini, lakini la msingi ni kwamba, kinywaji kikidhi haja ya afya ya binadamu. Kwa hiyo, tunawakaribisha wawekezaji na wajasiriamali, wawekeze katika eneo hili ili watengeneze kinywaji ambacho kinakidhi afya ya binadamu.

Na. 42

### **Upungufu wa Watumishi wa Afya Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ina upungufu wa watumishi 117 wa fani ya Afya kwa mwaka wa fedha 2007/2008; na kwa kuwa hadi sasa Halmashauri hiyo imepokea watumishi sita kati ya hao 117:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua kabisa tatizo hilo?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba upungufu huo mkubwa wa watumishi wa fani hiyo umeathiri kwa kiwango kikubwa huduma za Afya katika Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, ninaomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Mwongozo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Zahanati inapaswa kuwa na jumla ya watumishi watano, Kituo cha Afya kinapaswa kuwa na watumishi 29 na Hospitali ya Wilaya inapaswa kuwa na Watumishi wa Afya wapatao 154 wa kada mbalimbali.

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ina Zahanati 35 za Serikali ambazo zinafanya kazi. Zahanati nyingine kumi ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Aidha, Halmashauri hii ina Vituo vya Afya viwili na Hospitali moja. Hivyo, Halmashauri hii ilipaswa kuwa na watumishi wapatao 387 lakini watumishi waliopo ni 216 tu na hivyo kufanya upungufu wa watumishi wa kada zote kuwa 171.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya na inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa, suala la uhaba wa watumishi wa afya linapatiwa ufumbuzi. Miongoni mwa jitihada ambazo zinafanywa na Serikali ni pamoja na zifuatazo:-

- Kuondoa ada ya mafunzo kwa wanafunzi wanaochukua mafunzo ya udaktari ili kuvutia wanafunzi wengi waweze kusoma masomo hayo ya udaktari;
- Kufufua vyuo vya kada mbalimbali za afya ambavyo awali vilifungwa na pia tunatarajia kurejesha kada za afya zilizokuwa zimefutwa;-
- Serikali pia inatarajia kwamba watumishi walio na sifa kidogo watakuwa wanaendelezwa kwa awamu ili waweze kuwa na sifa zinazostahili na pia waweze kujaza nafasi wazi ambazo kwa sasa hazina wataalam.
- Serikali inaandaa programu ya mafunzo kwa watumishi wa afya kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuanzia mwaka 2007/2008.

Aidha Serikali imeweka utaratibu wa kuwapanga au kuwapatia ajira watumishi wa afya wanaotoka vyuoni moja kwa moja bila kufanya usaili, utaratibu ambao ulianza mwaka wa fedha 2005/2006. Pamoja na mkakati huu, imebainika kuwa wengi wa watumishi wanaopangwa vituoni, hawaendi kuripoti katika vituo walivyopangiwa kutokana na kile kinachodaiwa ni mazingira magumu ya kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba, upungufu wa Watumishi wa Afya umekuwa tatizo kubwa katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa, huduma bora za Afya zinatolewa kwa kila mwananchi. Ninaamini kabisa kuwa, jitihada za Serikali nilizozitaja, zitafanikisha kwa kiasi kikubwa azma ya Serikali.

Hata hivyo, ninaomba kutoa wito kwa Halmashauri zote kutengeneza mazingira mazuri ili watumishi wanaoajiriwa waweze kufanya kazi vizuri, hususan kujenga nyumba za watumishi karibu na maeneo yao ya kazi

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana alilitolea maelezo vizuri sana swali hili. Sasa kwa kuwa kuna vyuo vitano; Ngudu, Mpanda, Kagemu, Nachingwea na Iringa, ambavyo vilikuwa vinatoa mafunzo ya Maafisa wa Afya Wasaidizi; na kwa kuwa mafunzo hayo yalisitishwa; na kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kupanua vyuo hivi ili kufundisha waganga, yaani hawa *clinical officers*; je, mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Serikali ina azma ya kufufua vyuo vyote ambavyo vilikuwa

vimefungwa. Sasa vyuo ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge, navyo viko kwenye programu ya upanuzi pia kufufua hivyo vyuo ambavyo vilikuwa vimefungwa. Kwa hiyo, watumishi wote na kada zote ambazo tumeona kwamba zina upungufu zaidi, ndiyo watakaopewa kipaumbele kwenda kusoma katika vyuo hivi. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, hii ni programu ya muda mrefu na katika bajeti ya mwaka huu, programu hiyo imepewa kipaumbele.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba, sababu mojawapo inayosababisha watumishi kukimbia katika vituo vya kazi wanavyopangiwa ni pamoja na ugumu wa mazingira; na kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na wananchi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wamekwishaanza juhudi na wanaendeleza zile walizokwishaanza mapema; za kuhakikisha kwamba kutakuwa na zahanati katika vijiji na vituo vya afya katika kata; je, Serikali itakuwa tayari kushirikiana nao kwa karibu kuhakikisha kwamba katika mazingira hayo kunakuwa na nyumba za waganga na watumishi wengine, umeme, miundombinu muhimu kama vile barabara kufikika, simu na kuhakikisha kwamba maji yanapatikana ili kuweza kuwapa motisha hao wafanyakazi watakaopangwa katika vituo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali ya kwanza kabisa tumesema kwamba ni kuwapangia watumishi ambao wanamaliza katika vyuo moja kwa moja katika sehemu mbalimbali. Katika kutekeleza azma hiyo, tumeona kwamba ina mafanikio sana; wale ambao wanapangiwa moja kwa moja kutoka shuleni kuripoti katika vituo mbalimbali, wengi wao wameripoti. Kuhusu suala la kuboresha mazingira katika vijiji, ndugu zangu kama mnavyofahamu sasa hivi, miradi mingi sana tunaipeleka vijijini ndiyo maana kuna mradi wa barabara vijijini, mradi wa maji wa vijijini, mradi wa umeme vijijini ili kuboresha mazingira ya vijijini ili kuwavutia wafanyakazi wengi ambao wanaogopa kwenda huko vijijini.

Waheshimiwa Wabunge, tuseme moja; sote tumezaliwa vijijini na sote tumezaliwa katika mazingira magumu; mimi nitoe wito kwamba, mtu yeyote ambaye amepangiwa sehemu yoyote akubali kwenda huko. Sisi kama Serikali, hatutampangia sehemu nyingine tutahakikisha kwamba anaenda kule kule ambako amepangiwa.

Na. 43

**Ahadi ya Kutumia Makandarasi Kumalizia Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi imeanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuanzia na kilometa 36; na kwa kuwa mwezi wa tisa mwaka jana,

Serikali iliahidi kuwa itatumia makandarasi wawili tofauti kumalizia barabara hiyo: Je, Serikali itatimiza lini ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi, yenye urefu wa kilometa 115 ulikamilika mwaka 2006. Mkataba wa ujenzi wa barabara sehemu ya Mbeya – Lwanjilo yenye urefu wa kilometa 36, ulitiwa saina tarehe 1 Agosti, 2007 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na kampuni ya *Kundan Singh Contruction Limited* kutoka Kenya, kwa gharama ya shilingi 27,463,875,000.00. Muda wa mkataba ni miezi thelathini ukijumuisha muda wa miezi mitatu ya maandalizi ya kuanza kazi. Mkandarasi tayari yupo eneo la mradi tangu Septemba 2007 na kazi ya ujenzi wa barabara inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2008/2009, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu wa Lwanjilo – Chunya, yenye urefu wa kilometa 40. Kuhusu sehemu iliyobaki ya Chunya – Makongorosi yenye urefu wa kilometa 39, juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu hii zinaendelea. Aidha, sehemu hii itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida ya *TANROADS* ili iweze kupitika mwaka mzima bila matatizo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo yamenipa matumaini kuhusu barabara hii, nina maswali mawili ya nyongeza. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inasema kwamba, katika barabara hiyo pamoja na kujengwa kutoka Mbeya - Chunya hadi Makongorosi, katika kipindi hiki cha miaka mitano, vilevile kutakuwa na upembuzi yakinifu wa kutoka makongorosi kwenda Lupa - Matwiga hadi Itigi ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa lami kipindi kifuatacho cha utawala. Je, upembuzi yakinifu huo utanza lini?

Kwa kuwa mwaka 2006 mimi na Mheshimiwa Waziri tulitofautiana kidogo kuhusu barabara hiyo ya Mbeya, Chunya, Itigi, Manyoni, Babati kuwa ni sehemu ya *The Great North Road*; mimi nikisisitiza kwamba ni sehemu moja lakini Mheshimiwa Waziri akisema kwamba *Great North Road* ni ile tu inayotoka Mbeya – Iringa – Dodoma – Babati - Arusha kwenda Nairobi, lakini kwa bahati nzuri niliposafiri na Mheshimiwa Rais kwenda Scandinavia mwaka jana tukiwa Oslo; Mheshimiwa Rais akiongea wahisani aliitaja barabara hiyo kwamba *is part of the Great North Road*; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kurekebisha kumbukumbu ili kukuza historia?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kujenga barabara hiyo ya kutoka Mbeya mpaka Makongorosi hadi Itigi kama ambavyo tumeahidi katika ilani yetu. Kama tulivyoeleza, tayari barabara ya kutoka Mbeya hadi Makongorosi imeshawekewa mkakati wa

kujengwa kwa kiwango cha lami. Kutoka Makongorosi kuelekea mpaka Itigi, itafanyiwa maandalizi kama alivyosema ili katika kipindi kijacho nayo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu ni barabara kuu kwa maana ya *Truck Road* na dhamira yetu ni kwamba, barabara za *Truck Road* au barabara kuu ziwe zimejengwa kwa kiwango cha lami ndani ya miaka kumi ijayo. Kwa hiyo, hilo lipo kwenye mikakati ya Serikali na wala asiwe na wasiwasi.

Kuhusu ya barabara *Great North Road*, sidhani kama tulitofautiana; mimi nilisoma sheria ya mwaka 1961, inayoelezea vizuri hii *Great North Road* inapita wapi. Yeye alisema kumbukumbu ya historia, mimi nilisoma sheria ya barabara. Sasa kama kuna haja ya kubadilisha sheria, hatuna tatizo tunaweza tukarudisha tuibadilishe.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mwaka jana wakati tunapitisha *The Road Act*, Naibu Waziri alikuwa anasema kwamba, baada ya kupitishwa kwa sheria, basi zile barabara zinazotaka kupandishwa daraja, ikiwa ni pamoja na barabara ya kutoka Gulwe – Kibakwe – Chogora – Kinusi - Malolo hadi Ruaha Mbuyuni, nazo zitafikiriwa.

Sina hakika kama kupandishwa huko barabara zilizoombwa nchini kumefikia hatua inayoridhisha. Je, anaweza kutueleza kwamba masuala ya upandishwaji wa barabara hizo yamefikia wapi hasa hii barabara niliyoitaja?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli upandishaji daraja wa barabara haujafanyika na kuna ucheleweshaji. Kitu nilichogundua baada ya Sheria ya Barabara kupita ni kwamba, zinatakiwa *regulations* kadhaa ambazo zinatakiwa zitokane na sheria ile. Kwa hiyo, kwenye Wizara imeonekana kwamba, zile *regulations* inabidi zitengenezwe na wataalam wa ndani na wa nje wa Wizara. Sasa hivi Wizara inachofanya ni kujaribu kutafuta hao wataalam na kuwaweka pamoja, ili waweze kuangalia ni *regulations* gani zitakazotengenezwa kwa utalaam wa ndani na zipi zitengenezwe na wataalam kutoka nje.

Sasa katika kutengeneza zile *regulations* ndiyo itakuwepo pamoja na hiyo *schedule* ya barabara zipi zitapandishwa. Kwa hiyo, kazi hiyo imechelewa lakini ninaamini katika mwaka huu wa 2008, tutaendelea na zoezi hilo mpaka mwisho tuone tutakuwa tumefikia wapi. Tumechelewa lakini kazi inaendelea Wizarani, pale ambapo tutakuwa tumekamilisha basi tutajua kwamba ni barabara zipi zitapandishwa, kama ambavyo Wabunge wamekuwa wakiomba.

Na. 44

**Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu  
Julius Kambarage Nyerere**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-



Kwa kuwa kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita wananchi waliojenga kwenye maeneo ya Kiwalani/Kigilagila katika Jimbo la Ukonga waliagizwa kujiandaa kuondoka kwenye maeneo hayo na wasiendeleo na ujenzi au ukarabati wa nyumba ili kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kwamba watalipwa fidia: Je, ni lini sasa Serikali itatoa maelezo ya utekelezaji wa hatua hiyo ili kuwaondolea wasiwasi wakazi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, Ninapenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mwaka 1997 Serikali ilitia alama “X” katika baadhi ya nyumba za wananchi waliojenga kandokando ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere ili waondoke na upanuzi wa kiwanja hicho uweze kufanyika. Aidha, baada ya tathmini kufanyika, wananchi waliohusika waliagizwa wasiendeleo na ujenzi wa sehemu zao. Hata hivyo, tangu alama hizo ziwekwe hadi sasa ni miaka kumi na moja imepita na siyo miaka kumi na mitano kama Mheshimiwa Mbunge anavyodai.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kupanua Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere ili kiweze kuhudumia idadi ya abiria na mizigo inayopita kwenye Kiwanja, ambayo inaonyesha kukua mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, tatizo kubwa limekuwa ni namna ya kupata fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliojenga kandokando ya Kiwanja ili waondoke na kupisha upanuzi. Tathmini ya fidia kwa wananchi aliojenga kandokando ya Kiwanja kwenye mitaa ya Kipawa, Kigilagila na Kipunguni ilifanyika Septemba, 1997. Gharama ya fidia wakati huo ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 22. Gharama halisi kwa ssa (mwaka 2008) ni shilingi bilioni 28.

Katika kipindi chote, Serikali imeendelea na juhudi za kutafuta njia mbadala ya kupata fedha za fidia ikizingatiwa kuwa, fedha zinazotakiwa ni nyingi ikilinganishwa na majukumu ya Serikali. Njia mbadala iliyoonekana ingefaa ni kuwapata wawekezaji katika miradi ya kibiashara kama vile hoteli, maeneo huru ya biashara (*Export Processing Zone - EPZ*), ujenzi wa karakana za ndege, maghala ya mafuta ya ndege (*fuel farm*) na maduka ya biashara (*shopping malls*) na kadhalika, katika maeneo hayo. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, wawekezaji walialikwa na kupewa makabrasha ya zabuni ya miradi hiyo (*Request Proposals*). Hata hivyo, hakuna wawekezaji makini waliojitokeza. Kwa sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, inaendelea kuwasiliana na wawekezaji kadhaa wanaoweza kuwekeza katika Mradi wa Upanuzi wa Kiwanja hicho. Katika mazungumzo yanayoendelea, uwezekano wa wawekezaji kutoa pia fidia kwa wananchi hao (hasa wa mtaa wa Kipawa), kama mkopo kwa Serikali ama sehemu ya hisa zao unaangaliwa, sambamba na juhudi za Serikali kutenga bajeti ya fidia hiyo, angalau kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikishughulikia suala la fidia, Wizara imekuwa ikichukua hatua ya kuwapatia viwanja katika maeneo mengine, wananchi wote ambao watalazimika kuhama. Zoezi la kuwapatia viwanja linatekelezwa kwa awamu, ambapo kuanzia Agosti, 2007 wananchi wapatao 1,300 wa Kipawa na 300 wa Kipunguni ambao watahama, walianza kugawiwa viwanja katika eneo la Pugu Mwakanga, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, ili waweze kuviendeleza wakati wakisubiri kufidiwa na kuhamishwa. Zoezi hilo bado linaendelea na Mamlaka zinazohusika zinashughulikia upatikanaji wa hatimiliki kwa wananchi hao.

Aidha, Serikali inaendelea kulipa fidia kwa viwanja vingine 2,000 katika eneo la Pugu Mwakanga ili Wananchi wa Kigilagila na wale wa Kipunguni, ambao hawapo katika kundi lililopatiwa viwanja 300 waweze kugawiwa viwanja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, wananchi wanashirikishwa kikamilifu katika zoezi hili na wameunda Kamati ya kufuatilia mchakato mzima wa kugawiwa viwanja na hatimaye kulipwa fidia ya nyumba zao. Kamati hii imekuwa ikikutana mara kwa mara na watendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, pamoja na watendaji wa Wizara yangu, kwa lengo la kuhakikisha kwamba zoezi zima linafanywa kwa umakini na kukamilika vizuri.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo: Pamoja na majibu mazuri sana ya kuridhisha na kutia matumaini kwa wananchi wa eneo hilo, ninapenda niulize swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba itakuwa na mpango endelevu wa kulipa kidogokidogo kupitia Bajeti ya Serikali; je, mpango huo utanza lini ili angalau hao watu waweze kuondokana na adha ya kutokuwa na maendeleo kwenye maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza, tuna njia mbili; kwanza ni kujaribu kuweka kwenye bajeti angalau kwa awamu na nia ni kwamba, angalau tuanze na wale wa Mtaa wa Kipawa. Sisi kama Wizara, tutaweka tena mwaka huu hela zinazotakiwa angalau kwa Kipawa ambayo ni shilingi bilioni tisa. Sasa itategemea uwezo wa Serikali kuweza kutoa fedha hizo, kwa sababu kila mwaka tumekuwa tukijaribu lakini kutokana na majukumu ya Serikali, imekuwa inashindikana kutupatia fedha hizo. Kwa hiyo, tukizipata katika bajeti ya mwaka huu, basi tutalipa angalau wale wa Kipawa.

Hatua nyingine ni hii ya wawekezaji ambao wanataka kuuendeleza uwanja ule, tuzungumze nao ili kama wakikubali waingize fidia kwenye mradi ule; fidia ile inaweza kuwa ama hisa yao katika ule mradi kwa sababu itakuwa hisa ya Serikali na hisa ya hao

wawekezaji ama mkopo kwa Serikali, ambao tutazungumza tutaweza kurudishaje kwa hao wawekezaji. Kwa hiyo, njia mbili zote tunaziangalia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Bado tupo katika Wizara hiyo hiyo ya Miundombinu na swali sasa linaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani.

Na. 45

### **Hali ya Kivuko cha Pangani**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007 zilitengwa fedha kwa ajili ya Kivuko cha Pangani na taratibu za tenda zilifuatwa ingawa aliyeshinda zabuni alikiuka masharti na zabuni kufutwa; na kwa kuwa Benki ya Dunia imeshatoa barua ya kutokuwa na pinganimzi (*letter of no objection*):-

- (a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha zabuni mpya isitangazwe?
- (b) Je, Serikali itanunua lini injini mpya za kivuko cha sasa ili kifanye kazi vizuri bila kuhatarisha maisha ya Wananchi wa Pangani?
- (c) Je, itachukua muda gani kivuko kipya kufika Pangani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zabuni mpya haikuweza kutangazwa mapema kwa sababu kabrasha la zabuni lilitakiwa kufanyiwa marekebisho na kupata kibali kutoka Benki ya Dunia kabla ya kutanganzwa kwa zabuni. Hatimaye zabuni hiyo ilianza kutangazwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) tarehe 22 Oktoba, 2007 na ilifunguliwa tarehe 11 Desemba, 2007. Kwa sasa mchakato wa kumpata mzabuni wa kuleta kivuko hicho umekamilika na Wakala wa Barabara (*TANROADS*), wamepeleka tena Benki ya Dunia tarehe 1 Aprili, 2008 kwa ajili ya kupata kibali cha kusaini mkataba ili sasa huyo *supplier* aweze kuleta kivuko kipya.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa sasa haina mpango wa kununua injini mpya kwa ajili ya Kivuko cha Pangani. Hata hivyo, Wizara itaendelea kukifanyia matengenezo kivuko hicho kila inapotakikana, kuhakikisha kuwa kinaendelea kutoa huduma yake kama kawaida.

(c) Mheshimiwa Spika, kivuko kipya kitapatikana miezi kumi na mbili baada ya kutiliana saini na Mkandarasi wa kuleta na kujenga Kivuko hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu ya matumaini aliyoyatoa jana, ambayo Wananchi wa Pangani wameyapata, lakini leo Mheshimiwa Waziri ametoa majibu ambayo matumaini yameanza kufifia.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, suala la Kivuko cha Pangani, dharura ya sasa kwa muda wa mwaka mzima ni lazima tupate injini mpya kwa sababu tunahatarisha maisha ya wananchi mwaka mzima. Serikali wanasema hawataki kununua mashine mbili mpya; thamani ya roho za wananchi wale na injini mbili mpya ipi kubwa; mpaka tufe ndiyo tutaleta injini mbili mpya? Je, ni lini mtatunulia injini mbili mpya zifungwe katika Kivuko cha Pangani? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jitahidi umpunguze *pressure* Mheshimiwa Mbunge. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimpongeze kwa kweli kwa namna anavyofuatilia; ni kati ya Wabunge ambao ufuatiliaji wao katika matatizo ya wananchi wa majimbo yao ni mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeeleza kwamba, kwa mujibu wa *TANROADS* mwezi huu wa nne kabla ya mwisho, tutakuwa tumetiliana saini kuleta kivuko kipya na kwa maana hiyo, itachukua mwaka mmoja kivuko kipya kuja.

Mheshimiwa Spika, lakini kama unavyojua, kwa uzoefu tulionao, injini ya vivuko kama hivi, pamoja na *propeller* yake ambayo inatakiwa vilevile, unapoagiza mchakato ule wote si chini ya miezi sita; huendi tu kuchukua na kesho ukawa umeleta injini kwa maana kwamba, tukileta na kwa matatizo ya fedha tuliyonayo ni kwamba, hata hiyo injini itafika karibu na kivuko cheneyewe kipya kufika. Kwa hiyo, imeonekana ni busara kwamba, tuendeleo kutengeneza hapa, yaani kukarabati injini na boti ile na sasa hivi tumepata maombi ya shilingi milioni 35, kwa ajili ya kukiweka katika hali nzuri, hela ambazo wizara yetu itadhamini kwa sababu *TEMESA* wana matatizo kidogo ili feri ile iendeleo kufanya kazi kwa mwaka huu mmoja ambapo tunangojea feri mpya, kwa sababu kuleta injini nyingine itakuja wakati ambapo hiyo feri mpya nayo itakuwa inakaribia kufika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumetingwa na muda na sasa tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii; swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete.

### **Hifadhi za Taifa Tanzania**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aluliza:-

Kwa kuwa Hifadhi ya Kitulo iliyopo Makete ina vivutio vingi kama vile maua, ndege aina ya *Denhams Bustard*, mandhari nzuri na hali ya hewa nzuri; na kwa kuwa maua na ndege hao hupatikana kwenye msimu wa masika, yaani kuanzia mwezi Novemba hadi Aprili, misimu ambayo barabara zote zinazolingia na kutoka kwenye Hifadhi hiyo hazipitiki hivyo kufanya watalii washindwe kufika kwenye Hifadhi:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili hifadhi hiyo iweze kufikika majira yote?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ni miongoni mwa hifadhi mpya za Taifa zilizoanzishwa hivi karibuni. Hifadhi hii imeanzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 179 la tarehe 16 Septemba, 2005. Ni kweli hali ya barabara zinazolingia na kutoka kwenye hifadhi hii zinapitika kwa matatizo wakati wa msimu wa mvua. Pia ni kweli kuwa Hifadhi hiyo ina vivutio vingi vya utalii ambavyo ni vya kipekee kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Hifadhi hiyo ni mpya, hivi sasa Shirika la Hifadhi la Taifa la Tanzania (*Tanzania National Parks – TANAPA*), lina mkakati wa kuiendeleza kwa kuhakikisha kuwa hifadhi hiyo ina miundombinu muhimu kwa ajili ya shughuli za uhifadhi pamoja na utalii. Miundombinu ambayo imepewa kipaumbele kwa sasa ni ujenzi wa ofisi, nyumba za watumishi, pamoja na ile miundombinu ya kuhudumia wageni ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuna aina mbili za barabara zilizoko katika eneo hili la Hifadhi ya Kitulo; aina ya kwanza ni barabara ndogo ndogo zilizoko ndani ya Hifadhi, ambazo zinatumiwa na *TANAPA* kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na utalii. Matengenezo ya barabara hizi ni jukumu la *TANAPA*.

Aina ya pili ya barabara ni barabara kubwa zinazolingia na kutoka kwenye Hifadhi ya Kitulo ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Walaka wa Barabara (*TANROADS*), ambazo ni Chimala hadi Matamba na ile inayotoka Isyonje hadi Makete. Barabara hizi hutumiwa kwa shughuli za kawaida za jamii kama kusafirisha

abiria na mizigo, pamoja na kuleta watalii. Ujenzi na Ukarabati wa barabara hizi kwa kweli ni jukumu la *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kuwa ujenzi wa barabara hizi, yaani za kundi la pili ambalo nimesema kwamba ni jukumu la *TANROADS*, lakini kwa kuzingatia umuhimu wake kwa ajili ya shughuli za utalii, Wizara yangu itashauriana na Wizara ya Miundombinu ili kuzipa barabara hizi kipaumbele katika mipango yake kwa ajili ya kufungua eneo hilo kwa shughuli za utalii.

**MHE. DR. BINLITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupewa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, anayefanya biashara ya Utalii ni *TANAPA*, ambao wapo kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii; kwa hiyo, jibu la kwamba ni jukumu la *TANROADS*, ninadhani itakuwa si sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza ni lini hasa ukizingatia kwamba uwekezaji katika Hifadhi ya Kitulo ni mdogo ukilinganisha na uwekezaji kwenye machimbo ya madini ambako unahitaji Wataalam na hata vifaa, wakati kwenye Hifadhi ya Kitulo tunachohitaji ni barabara na mahali pa kulala wageni; ni lini Serikali itatumia fursa hizi ili kuwekeza katika Hifadhi ya Kitulo kwa kutengeneza miundombinu bora ili watalii waweze kufika katika sehemu hizi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Dr. Mahenge kwa *pressure* kubwa anayoiweka kwenye Wizara yetu kuhusu jambo hili. Ninajua jinsi ambavyo anapenda na amekuwa akisukuma maendeleo ya wananchi wake, kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali lake kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi, Wizara ya Maliasili na Utalii majukumu yetu makuu ni uhifadhi wa rasilimali zetu, lakini pia jukumu la pili ni la kuleta watalii. Kwa maana hiyo, fedha kidogo tunazokuwa tunazipata, tinalenga zaidi katika kuongeza idadi ya watalii wengi wanaoitembelea nchi yetu na hilo ndiyo lengo hasa ambalo tunahitaji kupimwa nalo. Suala la barabara sisi ni wanufaika tu lakini si jukumu letu la moja kwa moja. Labda nigusie kidogo kuhusu matatizo ya kifedha ambayo hifadhi hii inayo.

Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Hifadhi hii ya Kitulo ambayo imeanzishwa miaka mitatu iliyopita, haikuweza hata kupata mapato ya kuweza kujiendesha yenyewe, tulikisia kwamba, tutatumia shilingi 323,770,000; kati ya hizo Kitulo yenyewe tuliweza kukusanya shilingi milioni 13 tu ambayo ni asilimia nne tu. Kwa hiyo, mapato yanayokusanywa na Hifadhi kutokana na shughuli za *TANAPA* ni kidogo na hivyo inakuwa *subsidised* hata kwenye ule uendeshaji. Kwa hiyo, ukituongezea tena jukumu la kutengeneza barabara wakati hata shughuli ambazo ni za msingi hatuwezi kutokana na mapato tuliyonayo, kwa kweli unakuwa ni mzungu mzito.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, sisi ni wanufaika wakuu wa barabara hii, tutatumia *pressure* hii hii ambayo unaiweka kwetu kwa kushirikiana na kusaidiana na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu ili waipe kipaumbele barabara hii, kwa manufaa yetu sote kwani sisi sote tunahitaji watalii lakini na kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake ambao wanahitaji mawasiliano. (*Makofi*)

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, suala la utalii ni vizuri likaenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa tuna *Ruaha National Parks* ambayo hatupati watalii wengi kwa sababu ya barabara kuwa mbovu. Je, Waziri atakuwa tayari kushirikiana na Wizara inayohusika ili kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara inaboreshwa na kuhakikisha kwamba utalii unakwenda vizuri kwa sababu bila ya kuboresha miundombinu hata watalii tunaowazungumzia hawawezi kufika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kwa kifupi sana kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi na kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Mahenge kwamba, tunatambua umuhimu wa Barabara katika mawasiliano na katika kukuza utalii, kama moja ya vitu vya msingi kabisa. Kwa kuyatambua hayo, ndiyo nimekiri kwamba, tutashirikiana na wenzetu wa Miundombinu ili kuwaomba na kuwashawishi waipe kipaumbele Barabara hii ili watalii waweze kufika kwenye Hifadhi ya Kitulo.

Kwa hiyo, ninakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge ambalo tayari nilikuwa nimeshaahidi hivyo kwamba, tutashirikiana na wenzetu wa Miundombinu ili waipe kipaumbele na sote tunufaike.

**SPIKA:** Swali linalofuata linaulizwa kwa Wizara hiyo hiyo na Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini.

Na. 47

### **Msitu wa Sao Hill**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya Sera za Maliasili na Utalii ni kuweka mahusiano mema kati ya misitu ya Serikali na wananchi; na kwa kuwa kwa miaka mingi iliyopita mahusiano kati ya Wananchi wa Wilaya ya Mufindi na Msitu wa *Sao Hill* yalikuwa mazuri sana; na kwa kuwa ni miezi michache tu iliyopita msitu wa *Sao Hill* uliingia moto:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wasio waajiriwa walijitokeza kuzima moto huo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha Serikali ilikuwa imepata kwa kipindi cha Oktoba 2006/2007 na Oktoba 2007/2008?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), ninaomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Miti la *Sao Hill* lenye ukubwa wa Hekta 43,000 limeoteshwa kwenye eneo la nyasi za ukanda wa juu zilizoko katika Wilaya za Mufindi (asilimia 90), Kilombero (asilimia tano) na Kilolo kwa (asilimia tano). Katika kipindi cha kiangazi, nyasi hukauka kwa kipindi cha miezi sita. Kipindi hiki huwa na upepo mkali ambao husababisha uwezekano mkubwa wa moto kuenea na kuathiri eneo kubwa kama haukudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, matukio ya moto katika maeneo ya Mufindi ni mengi licha ya juhudi za kukabiliana nayo na yanatokea kutokana wananchi kutumia moto kutayarisha mashamba na shughuli nyingine za kujipatia kipato kama kurina asali au kuchoma mkaa. Moto mara nyingine huvuka na kuingia kwenye mashamba ya miti na hata makazi ya watu na kusababisha hasara kubwa. Wananchi wanaouzunguka Msitu wa *Sao Hill*, huelimishwa juu ya kuchukua tahadhari ya moto hasa nyakati za kiangazi, kupitia mikutano ya hadhara na semina au filamu kuhusu elimu ya mazingira. Hakuna mwaka ambao moto haujawahi kutokea ila athari zake hutofautikana kutokana na eneo na hali ya hewa ya siku moto ulipowaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli mahusiano kati ya Wananchi wa Wilaya ya Mufindi na Msitu wa *Sao Hill* ni mazuri sana na hii ni kati ya Sera za Maliasili na Utalii. Vilevile ni kweli kuwa, matukio ya moto katika maeneo ya Mufindi ni mengi licha ya juhudi kubwa za kukabiliana nayo. Katika tukio la moto la tarehe 25 Septemba, 2007, wananchi wasio waajiriwa waliojitokeza kuzima moto walikuwa 162 kutoka Kijiji cha Matama, ambacho kipo jirani na eneo lilioungua. Vilevile katika kuzima moto huo, watumishi wapatao 162 na askari 200 wa JKT Mafinga pia walishiriki.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Oktoba 2006/2007 na Oktoba 2007/2008, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi 6,495,833,302 kutokana na ushuru mbalimbali wa uvunaji wa miti katika Shamba la *Sao Hill*, ambapo shilingi 161,581,916 kati ya hizo zilikuwa ni ushuru kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Hii inatokana na ukweli kuwa, miti yote iliyovunwa katika kipindi hicho ilitoka katika eneo la Wilaya ya Mufindi Pekee.



**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Benito W. Malangalila.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonyesha kwamba ni wananchi 62 tu ndiyo waliojitokeza kwenda kuzima moto ule na idadi hii ni ndogo sana. Sababu zake zinafahamika kwamba, baada ya Serikali kupandisha sana bei ya msitu; uhusiano kati ya Wananchi wa Mufindi na msitu ule yaliharibika na ndiyo maana hawakujitokeza kwa wingi.

Ukiangalia mapato, Serikali imepata takriban shilingi bilioni sita na milioni mia tano na Wilaya ya Mufindi imepata shilingi milioni 161 tu. Je, Serikali haioni kwamba, Wananchi wa Mufindi waliopanda miti ile, wanaendelea kuzima moto kila siku; haya mapato ni kidogo sana kiasi kwamba inafaa tukubaliane kwamba tulipwe asilimia?

**SPIKA:** Mlipwe asilimia ngapi labda uwe wazi ili Waziri afahamu?

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Angalau asilimia mbili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ajili ya asilimia mbili.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye vipengele viwili, kama ifuatavyo: -

Kwanza, lile linalozungumzia kwamba wananchi waliojitokeza ni wachache na kwamba mapato inayopata Halmashauri ya Mufindi ni madogo. Labda nianze na hili kwamba, wananchi waliojitokeza ni wachache. Kwa takwimu tulizonazo ni kwamba, si wachache kwa maana kwamba eneo lenyewe lilivyo na hasa chanzo chenyewe cha moto, inavyoonekana kilianza kwenye eneo ambalo ni sehemu ambayo ni *quarters* za wafanyakazi. Kwa maana hiyo, sisi hatuna ushahidi wa moja kwa moja kwamba, wananchi hao walikuwa ni wachache.

Vilevile labda niseme kwamba, sidhani kama wale wananchi wenyewe ndiyo wamekuwa wakitozwa ushuru ule, kwa sababu ushuru huu umekuwa ukitozwa kwa wafanyabiashara wakubwa ambao ni wachache sana; ni wanavijiji wa pale.

Kwa maana hiyo na hii ni kwa ajili ya kuboresha mapato ya Serikali. Kwa hiyo, dhana ya kwamba kupanda kwa ushuru wa mazao ndiyo kulikosababisha wananchi kukasirika na hatimaye kutokutoa ushirikiano, mimi ninafikiri si sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushuru kwamba, Halmashauri ya Mufindi imepata kidogo, pia ninafikiri si sahihi kwa sababu kwanza hii shilingi milioni 161

niliyoisema ni ule ushuru wa Halmashauri, ambao unatozwa na kwenye maeneo mengine ambapo biashara inakuwa ikifanyika. Sasa ni vizuri nimwombe Mheshimiwa Mbunge na ni vizuri nimkumbushe faida za msitu huu kwenye eneo lake.

Faida za huu msitu pale Mufindi si hizi shilingi milioni 161 tu, Mufindi pale kuna faida nyingi ambazo wananchi wanazipata. Kwanza, hali ya hewa; sote ni mashahidi, upatikanaji wa maji na vyanzo vya maji ni vingi sana kutokana na uoto kuwa umehifadhiwa vizuri. Ukiacha misitu iharibike hali ikawa kama ilivyo Meatu, ndiyo hapo utakapojua kwamba, zile shilling milioni 161 pengine siyo *issue*; *issue* ni kwamba, uwepo wa msitu ule unaboresha mazingira na wananchi wananufaika kwa namna nyingi. Pamoja na kwamba maji yanapatikana lakini pia kuna vitu vingine vidogovidogo kama kuni, wanaruhusiwa wanaingia kwenye msitu kwa ajili ya kupata mazao ya misitu kama uyoga na matunda.

Kwa hiyo, niseme kwamba, kuna faida nyingi zinazotokana na misitu, pengine kulenga zaidi mawazo kwenye hii shilingi milioni 161 ambayo pengine inaweza ikawa si sahihi sana; kuna upana mkubwa wa faida inayopatikana na msitu huu kuwepo hapo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahamia sana katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini.

Na. 48

**Kupandisha Kiwango cha Mikopo ya Wanafunzi  
wa Elimu ya Juu**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa pendekezo la kupandisha kiwango cha mikopo kwa ajili ya chakula na malazi kutoka Sh. 2,500 hadi Sh. 3,500 kwa siku kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu limewasilishwa katika Baraza la Mawaziri ili kuidhinishwa:-

- (a) Je, wanafunzi gani walioshirikishwa katika mapendekezo hayo?
- (b) Je, ni lini suala hilo litaidhinishwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, lenye sehemu (a) na b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu wakati wa kufanya utafiti ili kubaini gharama halisi za malazi na chakula kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu, wadau mbalimbali walishirikishwa wakiwemo wanafunzi. Wanafunzi walioshiriki katika utafiti na kuandaa

mapendekezo ni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Ustawi wa Jamii, Chuo cha Elimu ya Biasahara (CBE) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT).

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kiwango cha fedha ya chakula na malazi kilikuwa Sh. 2,500 kwa siku; kiwango hicho kilipandishwa na Serikali kufikia Sh. 3,500 kwa siku mwaka 2006/2007. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la gharama za chakula na malazi, Serikali iliongeza kiwango hicho cha Sh. 3,500 hadi kufikia Sh. 5,000 kwa siku katika mwaka wa masomo wa 2007/2008.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mfumuko wa bei wa sasa ni mkubwa sana na kufanya Sh. 5,000 bado kutokidhi hali ya maisha; je, Serikali haioni sababu ya kuongeza kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 10,000?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa *means testing* ya kupata mikopo ina mlolongo mrefu; je, hatua gani za haraka zinachukuliwa ili wanafunzi wasiteseke kupata mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusiana na kuongeza Sh. 5,000= kuwa Sh. 10,000 kutokana na mfumuko wa bei; ukweli ni kwamba, kuna maeneo tumeshaongeza. Utakapofika mwaka wa fedha ujao kwa mfano, suala la *field* tutaongeza kutoka Sh. 6,000 mpaka Sh. 10,000, lakini inategemea katika bajeti tutapata kiasi gani ili tuweze kufikiria maeneo mengine. Tunakubaliana naye lakini inategemea pia hali halisi ya bajeti ijayo, lakini kwa uhakika tumeshaongeza eneo la *field*.

Mheshimiwa Spika, *means testing* haina mlolongo mrefu na ndiyo maana sasa hivi tumeshapeleka zile fomu mashuleni na katika vyuo husika, *form six* na wale walioko vyuoni wameshajaza. Hii yote ni kuhakikisha kwamba, wanazifanyia kazi ili wanapokuwa sasa wameshaitwa vyuoni, ile *means testing* matokeo yake yameshatoka na tumejua kiasi gani wanafunzi watalipwa ili kuharakisha malipo haya.

Na. 49

### **Uandaaji wa Walimu wa Kutosha**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kuandaa walimu wa kutosha watakaokidhi kero ya uhaba wa walimu katika shule za msingi na za sekondari nchini:-

Je, walimu wangapi kati ya hao wanaoandaliwa wataweza kutosheleza huduma kwa watoto wanafunzi wenye ulemavu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Taifa linakabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu katika Shule za Msingi na Sekondari. Wizara yangu inatekeleza Mpango Kabambe wa Mafunzo ya Walimu ili kukidhi mahitaji ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, zikiwemo shule za wenye ulemavu. Mpango huo unatekelezwa kwa kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo katika Ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada na kuanzisha vyuo vipya. Kwa mwaka huu 2007/2008, walimu wanafunzi walioko vyuoni Ngazi ya Cheti kwa ajili ya kufundisha Shule za Msingi ni 9,557, wanachuo watakaofundisha Shule za Sekondari (ngazi ya Stashahada) ni 5,959 na wanaosomea Shahada ni 2,843. Mitaala inayotumika kuwaandaa walimu hao ni ya Elimu Jumuishi, ambayo inalenga kuwajengea uwezo walimu wote kufundisha wanafunzi mchanganyiko darasani (wasio na ulemavu na wenye ulemavu). Mitaala hiyo inasaidia kuondoa ubaguzi katika utoaji wa elimu na kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za wenye ulemavu kwa sasa ni 1:25, lengo ni kufikia uwiano unaotakiwa wa 1:10. Kwa hiyo, mahitaji ya walimu katika shule hizo bado ni makubwa. Hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali za kuwanda walimu hao ni pamoja na kuongeza nafasi katika Chuo cha Ualimu Patandi. Chuo hiki kinatoa mafunzo kazini ya kuwaimarisha zaidi walimu katika kufundisha na kutoa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kimeanzisha mafunzo ya Walimu wa Elimu Maalum katika ngazi ya Shahada. Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa, vitaanza kutoa mafunzo hayo mwaka 2008/2009. Kwa sasa walimu walioko mafunzoni ni 425; wakiwemo 288 wa Ngazi ya Cheti, 102 wa Stashahada na 35 wa Shahada.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri yanayotia moyo lakini nina maswali mawili. Ninashukuru kwamba, kuna vyuo vitaendeleza suala hili lakini kwa sasa hivi ni Chuo cha Patandi tu ndiyo kinachoimarisha mafunzo haya ya watoto wenye ulemavu. Sasa je, ni lini Patandi itaanza kuongezewa miundombinu na wakufunzi ili ikidhi haja ya Serikali iliyoitamka hapa?

Mheshimiwa Spika, la pili, wanachuo wanaotoka Patandi sasa hivi kwa sababu ndiyo chuo pekee hao wengine wata, wata, wata, lakini Patandi inaendeleza haya; ni kwamba wanafunzi wanaotoka Chuo cha Patandi wanaporudi kwenye maeneo yao inakuwa vigumu kupandisha vyeo baada ya mafunzo ya miaka miwili; hivi hili linasababishwa na nini kwa sababu wao hukatishwa tamaa katika utendaji wao wa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Chuo cha Patandi pekee ndicho ambacho kinatoa mafunzo maalum. Kama tulivyosema, vyo vyote tofauti na ilivyokuwa hapo zamani, sasa hivi wanachuo wanafundishwa elimu mjumuisho, yaani watakapotoka katika chuo watakuwa wamehitimu jinsi ya ku-*handle* wanafunzi wasioona, wasiosikia na wenye mtindio wa akili katika madarasa yao mjumuisho. Kwa hiyo, sasa hivi kila shule itahudumiwa kwa wale wenye ulemavu. Ni kweli Patandi miundombinu haitoshi na hilo Serikali tumeshaliona, tutalifanyia kazi kwa kuwa ni Chuo chenye vifaa kwa ajili ya elimu maalum, basi kiongezewe na idadi ya wanafunzi kwa ajili ya elimu maalum, hasa kwa ajili ya shule zile ambazo zinachukua wanafunzi wa elimu maalum pekee ambazo siyo shule mjumuisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vyeo, suala la upandishaji wa vyeo kwa walimu ni sawa na wafanyakazi wengine, inategemea mambo mengi. Inawezekana walimu hawajazi fomu husika na hawafuati taratibu. Kwa hiyo, ninafikiri hili siwezi kulijibu kwa ujumla kwamba ni kuhusiana na hawa walimu wanaokwenda kusoma Patandi, lakini ninafikiri linahitaji kuwasiliana na walimu wale watupe taarifa ni nani ambaye hajapandishwa cheo baada ya kusoma na kama ile kozi ilikuwa inahitaji kupandishwa cheo baada ya kusoma.

Na. 50

### **Ukosefu wa Maji Kata ya Old Moshi Magharibi**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni uhai;na kwa kuwa Wnanchi wa Kata ya *Old Moshi* Magharibi, Vijiji vya Korini Kusini wamekosa maji kwa miongo miwili sasa huku kisima kilichojengwa hapo tangu miaka ya 1980 kikiwa hakina maji, wala hakijawahi kuwa na maji:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu hali hiyo hasa ikizingatiwa kuwa hata Mto Mrusunga ambao ulikuwa unategemewa umekauka kabisa na Mto Rau pia nao unatishia kukauka na uko mbali na wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Korini Kusini kipo katika Kata ya Mbokomu yenye Vijiji vitatu vya Tema, Korini Kaskazini na Korini Kusini. Mwaka 1980 miradi miwili ya maji ya Mbokomu Mashariki na Mbokomu Magharibi, ambayo vyanzo vyake vya maji ni chemchemi za Mrusunga A na Mrusunga B zilizopo kwenye Misitu ya Kitaifa ya *KINAPA*, ilijengwa ili kutoa huduma ya maji kwa vijiji hivyo. Kutokana na ongezeko la watu katika maeneo hayo na miradi hiyo kuwa ya miaka mingi, maji hayo kwa sasa

hayatoshelezi mahitaji ya wananchi wa Kata husika, hususan Kijiji cha Korini Kusini. Hali hii imesababisha tanki la maji lililojengwa Korini Kusini, kutopata maji ya kutosha kukidhi mahitaji ya kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la maji katika Kijiji cha Korini Kusini, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ilibuni Mradi wa Maji ya Mtiririko kutoka chemchemi ya Maruweni iliyopo Kijijini Tema, kwa nia ya kuongeza wingi wa maji yanayotoka kwenye Mradi wa Maji wa Mbokomu Mashariki. Mradi huo unaotumia maji ya chemchemi ya Maruweni ulibuniwa kama hatua ya muda mfupi. Mradi huo ambao ulianza kutekelezwa mwezi Agosti, 2007 ni miongoni mwa miradi ya maji inayotekelezwa katika Wilaya ya Moshi Vijijini, chini ya Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mradi huu upo kwenye hatua za mwisho za utekelezaji. Hadi hivi sasa, ujenzi wa chanzo cha maji cha Maruweni chenye uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 21.6 kwa saa na matanki matatu ya kupunguza nguvu ya maji (*break pressure tanks*), yenye vilula vya kuchotea maji tayari umekamilika. Aidha, ufungaji wa mabomba yenye urefu wa kilometa tano na ukarabati wa vituo vya kuchotea maji viwili umekamilika na vinafanya kazi. Ukarabati wa vituo vya zamani vinne vya kuchotea maji unaendelea. Hivi sasa maji kutoka kwenye mradi huu yanaingia kwenye tanki la mwisho na Wananchi wa Korini Kusini wanapata huduma ya maji kutoka kwenye mradi huu, ambao ulizinduliwa rasmi tarehe 19 Machi, 2008, wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji. Vijiji vya Tema na Korini Mashariki, vinatarajiwa kupata huduma ya maji ya kutosha baada ya kukamilisha kazi ya kuzibua mabomba ya mtandao wa zamani ifikapo mwisho wa Aprili, 2008.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2007 Serikali ilitoa Sh. 38,035,500 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji na kazi inaendelea. Aidha, ninapenda kuwapongeza Wananchi wa Korini Kusini kwa mchango wao wenye thamani ya Sh. 4,600,000 kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Maji wa Korini. Kuhusu kukauka kwa Mito ya Mrusunga na Rau, ninapenda kutumia nafasi hii kuzikumbusha Halmashauri zote za Manispaa, Wilaya na Miji, kusimamia kikamilifu Sheria na Sheria Ndogo zinazohusu uharibifu wa vyanzo vya maji. Kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya maji bila kuhifadhi vyanzo vya maji, hakutakuwa endelevu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, Wananchi wa Korini Kusini wanapata maji katika mradi uliozinduliwa mwezi Machi, 2008. Mimi nimetoka huko na ni kweli kwamba, wananchi wale mpaka sasa hivi hawana maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kutokana na tatizo kubwa lililopo pale; Mheshimiwa Waziri au Naibu wake wapo tayari kuongozana na mimi kwenda kuona ukubwa wa tatizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nianze na la pili. Nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Lyimo, tukakague hali ilivyo katika Kijiji hicho. Ninapenda nimhakikishie kwamba na mimi ni mdau, ningependa nione zaidi maendeleo ya maji katika Kata hii. (*Kicheko*)

Kuhusu kwamba wananchi hawana maji, ninaomba tu Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba, katika jibu langu nimesema tunaendelea na kazi nyingine ya kukamilisha kabisa mradi ule wa maji. Hiyo kazi inaendelea na fedha tumekwishapeleka, lakini kama nilivyosema, nipo tayari tutakwenda kuangalia kama kuna upungufu basi mradi huo nina hakika utakamilishwa.

Na. 51

### **Programu ya Taifa ya Maji Safi na Salama Vijijini**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwepo na Programu ya Maji Safi na Salama kwa wananchi na ule mpango uliomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 – 2010 kwamba asilimia sitini na tano ya maji safi na salama yafikishwe kwa wananchi vijijini:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni asilimia ngapi hadi sasa imeshatekelezwa kwa nchi nzima?

(b) Kwa kuwa mpango wa kufikisha maji safi na salama kwa wananchi kwa asilimia 65 unategemea sana fedha za wahisani kama vile *World Bank (WB)*, *ADB*, Mashirika ya Dini na kadhalika; na kwa kuwa moja kati ya masharti ya *World Bank* ni uchangiaji wa asilimia kumi za mradi; na kwa kuwa mradi hupangiwa vijiji kumi kila mwaka kwa kila Wilaya; je, kwa nini hadi sasa miradi yote ya awamu ya kwanza haijakamilika kama vile ile iliyoko Jimboni Iramba Magharibi ya Kiomboi, Mampanta, Misigiri na Mkulu na ni lini awamu ya pili itaanza kwa Vijiji vya Ndago (Nguvumali), Ng'anguli na Mlandala?

(c) Je, ni miradi mingapi ya *Quick Win* ilitolewa Jimboni Iramba Magharibi kwa mwaka 2007/2008?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, kwa uhakika kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Desemba, 2006 asilimia 55.7 ya wakazi wa Vijijini, walikuwa wanapata huduma ya maji safi na salama kwa nchi nzima. Mwaka 2003, Serikali ilianzisha Mradi (*Pilot Project*) wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Wilaya za Rufiji, Kilosa, Mpwapwa, Kiteto, Kongwa, Morogoro Vijijini, Mvomero, Handeni, Kondo, Singida Vijijini, Iramba, Igunga, Kilindi na Manyoni, kwa lengo la kujifunza na kutumia uzoefu wa mradi huo katika kutekeleza programu ya kuendeleza

sekta ya maji, ambayo kwa sehemu kubwa inategemea fedha za nje. Katika juhudi za kupunguza kero za wananchi, Serikali iliamua kuanzisha utekelezaji wa Miradi ya *Quick Wins* isiyohitaji kufanyiwa usanifu wa kina na fedha nyingi katika muda mfupi. Halmashauri 84 zilizokidhi vigezo kati ya 121, zilipata fedha na kuanza kutekeleza miradi yao ya maji na utekelezaji unaendelea. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba, ifikapo mwaka 2010 asilimia 65 ya wananchi wanaoishi vijijini wanapata maji safi na salama.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Wilaya ya Iramba ulianza mwaka 2005. Maeneo yaliyohusika katika Jimbo la Iramba Magharibi ni Kiomboi, Mampanta, Misigiri na Mkulu. Sababu zilizocheleweshwa kukamilika kwa miradi ya maji ni ukosefu wa maji katika baadhi ya visima vilivyochimbwa na hivyo ilibidi kurudia uchimbaji katika maeneo ya Msigiri, Nselembwe, Mlandala, Kiomboi na Gumanga ili kupata maji. Hadi Aprili, 2008 hakuna maji yaliyopatikana katika Vijiji vya Mlandala na Gumanga. Vijiji hivyo vitaingizwa kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ili utafiti zaidi wa vyanzo vya maji ufanyike. Katika Vijiji vya Msigiri na Kiomboi, maji yamepatikana na mradi utakamilika mwezi Juni, 2008. Aidha, mradi katika Kijiji cha Nselembwe unafanya kazi, ambapo watu 7,500 wanapata huduma ya maji safi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini utafikia ukomo wake mwezi Juni, 2008. Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mlandala ambao haukukamilika kutokana na ukosefu wa chanzo cha maji, pamoja na Vijiji vya Nguvumali na Ng'anguli, itatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Utekelezaji wa miradi hiyo utanza mwaka 2008/2009, baada ya kumpata mtaalam mshauri atakayefanya kazi ya uhamasishaji, usanifu na usimamizi wa miradi. Utafiti zaidi utafanyika ili kubaini vyanzo vingine vya maji kwa ajili ya vijiji hivyo.

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi midogo sita katika Jimbo la Iramba Magharibi inatekelezwa mwaka huu wa 2007/2008, kwa kutumia fedha zilizotolewa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Miradi hiyo ni ya Vijiji vya Masagi, Lunsanga, Uwanza, Kyalosangi, Mtekente na Makunda, ambapo utekelezaji upo katika hatua za mwisho. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilitumia Sh. 103,003,500 kwa ajili ya vijiji hivyo, kati ya Sh. 144,100,000= zilizotumwa kwenye Halmashauri hiyo.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini akiwa amechanganya changanya vijiji; nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Miradi aliyoisema ya Kiomboi, Mampanta, Misigiri na Mkulu ilikwenda pamoja na ule Mradi wa Nselembwe, ambao umekwisha na ukaanza kazi takriban mwaka mmoja uliopita na mradi huu pamoja na hiyo niliyoitaja ilikuwa kwa pamoja ije izinduliwe na aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati ule, Mheshimiwa Edwara Lowassa; na maji yalikuwa tayari yameshapatikana na mtandao ulishafanywa wa umeme na vitu vingine ambapo kila kitu kilikamilika; je, ni sababu zipi zilizofanya kwa mwaka mzima hadi sasa wananchi wa vijiji hivyo wasipate maji?



Swali la pili, kwa kuwa amesema Programu ya Miradi ya Maji Safi Vijijini ilianza mwaka 2005/2006 huko Iramba lakini mwaka 2006/2007 hakuna utekelezaji wowote uliofanyika; sasa ili tufikie hiyo asilimia 65; je, Wizara ipo tayari kufanya kwa mkupuo miradi miwili ule wa 2006 na 2007 kwa mwaka 2008/2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi, yapo matatizo ya utekelezaji ambayo mengine yalikuwa nje ya uwezo wetu, kwa mfano, nimesema kutopatikana kwa maji, lakini pale ambapo maji yamekwishapatikana na suala lilikuwa la utekelezaji, kilichobaki sasa ni kufuatilia. Ninajua yapo matatizo ambayo yamejitokeza katika utekelezaji wa miradi hii ya maji. Yapo hata matatizo ya uwezo wa ku-*absorb* hizi fedha katika kutekeleza kazi hizi; haya yapo katika Wilaya, kwa hiyo, tunachokifanya sasa hivi ni kujaribu kuziwezesha Wilaya ili ziweze kutekeleza miradi hii kwa uwezo kabisa na kwa haraka zaidi. Hili tatizo tunaendelea nalo na hatuwezi kulitatua mara moja.

Nikizungumzia habari ya mtandao wa maji ambao ulikwishakuwa tayari unachosubiri ni kuzinduliwa, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Killimbah kwamba, nitalifuatilia suala hili kwa kuwa fedha zilikwishatolewa mwaka 2006/2007 na kuangalia ni nini hasa kilichosababisha kutokamilika kwa miradi hiyo.

Hilo ninaamini kwamba, tutalitolea majibu kwa sababu 2007/2008, hatujapata fedha za kutekeleza miradi hiyo, kwa sababu kwanza ni viporo ambavyo havijakamilika. Kwa hiyo, tunataka kwanza tutoe kipaumbele kwa miradi ile ambayo tayari imekwishapewa fedha. Mwaka 2007/2008, sasa mchakato wake wa kupata fedha ndiyo unaoendelea.

Nimalizie kwa kusema kwamba, mchakato wa kupata fedha hizi zinazotoka nje siku zote, hauwezi kwenda kama tunavyopanga kwamba, tunataka mwezi wa Sita ufike mwezi wa Sita, ndiyo maana bado tunaendelea na mchakato wa kuomba vibali kutoka *World Bank* ili fedha ziweze kupatikana. Ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitafuatilia hilo suala ambalo Waziri Mkuu alikwishapita huko akaliona na akaahidi kwamba mradi ungezinduliwa.

Na. 52

### **Tatizo la Msongamano wa Mahabusu Magerezani**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI** aliuliza:-

Kwa kuwa mahabusu na wanaowatuhumu katika maeneo mengi wamekuwa wakitakiwa kulipia gharama za kwenda Mahakamani na gharama za Mgambo au Askari wa kuwapeleka Mahakamani, jambo ambalo linasababisha msongamano wa Mahabusu katika Magereza mengi: Je, Serikali itatatuaje tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *The Prisons Act, Cap. 58, R.E 2002* na *Magistrates' Courts Act, Cap. 11, R.E. 2002*, Wafungwa na Mahabusu ambao wako rumande kutokana na amri ya Mahakama, wote wapo chini ya uangalizi wa Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza ndilo lenye wajibu kisheria kutoa huduma kwa wafungwa na mahabusu, ikiwemo kuwapeleka Mahakamani na kuwarudisha rumande, chakula, huduma za matibabu na huduma nyingine ambazo zimeainishwa katika Sheria tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria inayounda Jeshi la Polisi (*Police Force and Auxiliary Service Act, Cap 322 R.E 2002*) kifungu cha (5), Jeshi la Polisi ndilo lenye wajibu wa kumkamata mtuhumiwa na kumpeleka Mahakamani kwa mara ya kwanza au kwa amri ya Mahakama. Pamoja na kwamba jukumu la kusafirisha mahabusu walioko Magerezani kwenda Mahakamani na kuwarudisha gereza kisheria ni la Jeshi la Magereza, kwa sasa Jeshi la Polisi ndilo linalowasafirisha mahabusu. Hata hivyo, Jeshi la Magereza lipo katika mchakato wa kutekeleza jukumu hilo kama sheria inavyoelekeza. Pale inapotokea eneo alilopo mtuhumiwa hakuna Kituo cha Polisi na anatakiwa kufikishwa Mahakamani, Uongozi wa Serikali ya Kijiji au Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, anatakiwa kuteua Askari Mgambo au Tarishi wa Mahakama, kuwapeleka watuhumiwa Mahakamani au Gereza. Gharama za kuwalipa Askari Mgambo au Tarishi wa Mahakama, zinalipwa na Mkuu wa Gereza husika baada ya Hakimu kumwandikia Mkuu huyo wa Gereza awalipe wasindikizaji hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo: Kama nilivyotanabahisha katika maelezo yangu ya utangulizi; ni jukumu la Serikali kugharamia gharama zote katika makosa ya jinai ikiwemo kuwakamata watuhumiwa, kuwafikisha Mahakamani, kuwapeleka rumande, kuwalipa mashahidi, walalamikaji, Wazee wa Baraza na huduma nyinginezo. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba kutoa Rai kwa wananchi wote kwamba, hawatakiwi kulipa gharama yoyote ile kwa Askari Polisi, Askari Mgambo au Tarishi wa Mahakama, wanaposhiriki kumkamata mtuhumiwa na kumfikisha Mahakamani au Gereza. Hata hivyo, iwapo wapo baadhi ya Askari Polisi, Askari Mgambo au Tarishi wa Mahakama, ambao hudai malipo kwa kutekeleza wajibu huo, basi wanakwenda kinyume cha Sheria na Taratibu. Hivyo, wananchi wasisite kutoa taarifa katika vyombo vya Serikali katika maeneo yao ili hatua za kinidhamu na kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao ili kumaliza tatizo hili kama lipo.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninashukuru kwa majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni mazuri

kinadharia lakini utekelezaji wake haupo, tatizo hili ni kubwa sana. Sasa ninataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; je, atakuwa tayari kufanya utafiti katika maeneo mengi hasa kwenye ngazi za Wilaya na Vijiji kwamba hali hii haipo kama anavyoeleza yeye ni tatizo kubwa na ni kero kwa wananchi? (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa, kutokana na tatizo hilo kuna mahabusu 17 waliokufa kwa kukosa hewa katika mahabusu ya Kituo cha Polisi na Serikali iliahidi kutoa kifuta machozi kwa wale waliofiwa kwa maana ya wajane na ndugu na ilisubiriwa kesi iishe na kesi hiyo imekwisha: Je, Serikali bado ina azma hiyo ya kutoa kifuta machozi na kama kipo, ni lini watafanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo ambalo nimejaribu kujibu katika suala la msingi. Ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kusema kwamba tatizo hilo bado lipo na kama alivyoomba kama nipo tayari au Wizara yangu ipo tayari kushiriki na kufanya utafiti na kuona kwamba hilo tatizo lipo katika ngazi ya Wilaya na vijiji, nataka kumshukuru na kumhakikishia kwamba hizi ndizo kazi ambazo tupo hapa kuzifanya kwa kuwasikiliza wawakilishi wa wananchi kupata vilio vyao na matatizo yao na ninaahidi kwamba tutalifanyia utafiti na tutalifanyia kazi. Kwa kweli kama lipo, tutajaribu kutafuta njia za kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mahabusu ambao walifia gerezani 17, ni kweli Wizara inalitambua tatizo hilo na lilikwenda Mahakamani na bado linafanyiwa utaratibu wa kuona ni jinsi gani uamuzi wa Mahakama utatekelezwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona tumalizie swali la mwisho kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili yale maswali mawili ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi basi yasogezwe mbele. Kwa hiyo, namwita sasa Prof. Feetham Banyikwa - Mbunge wa Ngara.

Na. 53

### **Hali ya Wafanyakazi *Rusumo Border***

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji katika Kituo cha *Rusumo Border* Wilayani Ngara wanafanyakazi katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na kuwa na Ofisi ndogo sana na kukosa gari la kazi:-

Je, Serikali itawaboreshea lini mazingira ya kazi ili wasiendee kulundikana katika Ofisi hiyo ndogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua matatizo yanayoikabili Idara ya Uhamiaji ikiwemo uhaba wa Ofisi na nyumba za watumishi, upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari, pikipiki na samani katika maeneo mbalimbali hapa nchini kikiwemo Kituo cha Uhamiaji Rusumo. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ufinyu wa Ofisi, uhaba wa vitendea kazi na nyumba za watumishi unawafanya Watumishi wa Idara hii kuwa katika mazingira magumu ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotanabaisha katika bajeti yangu niliyowasilisha katika Bunge lako Tukufu tarehe 31 Julai, 2007, nilieleza malengo ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Malengo hayo ni pamoja na kuzifanyia ukarabati na upanuzi Ofisi katika vituo mbalimbali hapa nchini. Katika mpango huo wa upanuzi na ukarabati wa Ofisi na Vituo vya Uhamiaji, Kituo cha Rusumo ni miongoni mwa vituo vitakavyofanyiwa upanuzi wa Ofisi na ukarabati wa nyumba wanazoishi watumishi.

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa upanuzi wa ofisi na ukarabati wa nyumba za watumishi katika vituo mbalimbali kikiwemo cha Rusumo na upatikanaji wa vitendea kazi yakiwemo magari, pikipiki na samani za ofisi utafanyika kwa awamu kadri bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008 itakavyoruhusu. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele kitaendelea kutolewa kwa ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Uhamiaji Rusumo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Banyikwa kidogo ulipatwa na butwaa. Swali la nyongeza!

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, wakimbizi wanaondoka mwezi Juni, 2008 na Ofisi ya *UNHCR* ina magari mengi ya *Landcruiser* na Ofisi za Polisi Kabanga na Rusumo hazina usafiri, kwa nini magari hayo ambayo yapo kwenye Ofisi ya *UNHCR* zisipewe Ofisi hizo ili ziweze kutatua matatizo ya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *UNHCR* wamo mbioni kumaliza shughuli zao katika eneo la wakimbizi kule Ngara na ni kweli kwa mujibu wa ufahamu wangu kwamba *UNHCR* wana magari yao ambao wanayauza kwa mnada.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kusema tu kwamba Serikali huwa hainunui magari ambayo yamekwishatumika, kwa kuwa sera ya Serikali ni kununua magari ambayo ni mapya. Lakini kwa kuwa suala hili nadhani Prof. Banyikwa alikwishakulizungumza mahali na nilikuwa na habari nalo ni kiasi cha kuzungumza na kama tunaweza tukapewa kama msaada kwa kweli tutakuwa hatuna tatizo nalo. Lakini ninamwomba Mheshimiwa Mbunge atuelewe kwamba sio sera ya Serikali kununua magari ambayo yamekwishatumika. Lakini kwa kuwa *UNHCR* wamekuwa

wanatufanyia kazi nzuri kwa ushirikiano mzuri na kama inaweza ikatokea fursa hiyo kwamba tunaweza tukapata msaada wa magari kutoka kwao ili sehemu kama hizo za Uhamiaji na Polisi waweze kuyatumia katika maeneo ya Rusumo, nadhani hilo ni suala ambalo ningeomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalitazama bila tatizo lolote. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumebakiza maswali mawili ambayo yatajibiwa wiki ijayo. Muda wa kipindi cha maswali umekwishapita, sasa ni matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza, ninafurahi kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge na pia kuwashukuru kwamba mchango wetu sisi Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya Mfuko wa Maafa ya Mererani kufikia leo asubuhi umefikia shilingi milioni 17,545,000/=. Ninaona kwa sababu juhudi zinaendelea, ni vizuri basi fedha hizi zilizokwishakupatikana wiki ijayo zikabidhiwe Ofisi ya Waziri Mkuu zote Sh. 17,545,000 ili ziende kule Mererani kusaidia baadhi ya matatizo yaliyopo kule. Tunaendelea kuwapa pole sana wahanga wote wa maafa ya Mererani na Bunge hili lipo nao kama lilivyo na wananchi sehemu zote ambao wanapata matatizo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu wageni, orodha ya kwanza ya wageni ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha ambao ni wafuatao: Ndugu Mohamed Mmuya Katibu Mkuu nadhani atakuwa pale. Katibu Mkuu Mmuya, yule pale ahsante sana na karibu sana; Bibi Aginela Nyoni ambaye ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hongera sana. Sio rahisi katika mfumo dume huu kupenya na kupata Ukuu wa Idara. Nakupongeza sana Mama Nyoni. Bwana Joseph Konyo Mratibu wa Polisi Makao Makuu yule pale na Bwana John Mgunda - Mhasibu wa Wizara. Inawezekana yupo huku.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo ambao ni Dick Manongi - *Dean of Students* Chuo Kikuu cha Dodoma na watoto wake Nathan na Joseph.

Waheshimiwa Wabunge, wapo Maafisa 20 wa Maendeleo ya Jamii ambao walikuwa kwenye mafunzo kuhusu uratibu na usajili wa Taasisi zisizo za Kiserikali. Maafisa Maendeleo ya Jamii, wale pale. Karibuni sana na ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo la kuwepo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Ludovick Utouh akifuatana na Maafisa 16 kutoka kwenye Ofisi yake yule pale na Maafisa wapo upande wangu wa kulia. Ndugu Ludovick Utouh Bunge hili linafarijika sana na kazi nzuri uliyoifanya ya ukaguzi wa hesabu za Serikali. Tukuomba uwe imara usitishike ni kazi ngumu na wenzako pia waendeleo na kazi hiyo ngumu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 20 wa Shule ya Sekondari Mvumi Makuru ya Jimbo la Mtera ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dr. John Malecela. Wale

pale na walimu wao tunawapongeza sana kwa kuwaleta vijana ili kuona demokrasia yao ikifanya kazi hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wanafunzi 20 kutoka Shule ya Sekondari ya Azimio Dodoma, wale pale! Ahsante pamoja na walimu, karibuni sana, msome kwa bidii, Tanzania inaendelea kuhitaji watu wenye kusoma vizuri na wawe na stadi za kutosha kwa sababu nchi inazidi kuendelea na inahitaji wasomi wazuri. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kuwatambulisha wenzetu wa Kampuni ya *NICOL*. *NICOL* ni Kampuni ambayo inajitahidi kuwahamasisha Watanzania wazalendo kuwekeza katika uchumi. Yupo ndugu Felix Masha - Mwenyekiti wa Bodi, naomba upunge mkono ndugu Felix. Yule pale, yupo kaka yangu Ibrahim Kaduma - Mjumbe wa Bodi, yule pale; Engineer Mark Mjiu - Mjumbe wa Bodi; Martha Quoro - Mjumbe wa Bodi - Paul Makanza Mjumbe wa Bodi, Leo Akunai - Mtunza Hesabu na Fedha na Maganga Mwajasho - Mwanasheria. Ahsanteni sana na tunashukuru sana kwa kazi mnayoifanya. Ni kweli uchumi hatimaye lazima ushikwe na wananchi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, kuambatana na hilo, Kampuni ya *NICOL* imetoa mwaliko ili tuhudhuria hafla itakayofanyika katika Ukumbi wetu pale wa Viwanja vya Bunge kuanzia saa 2.00 usiku leo. Kutakuwa na mambo ya kawaida yanayohusiana na hafla, lakini kubwa zaidi Mwenyekiti wa Bodi atatumia fursa hiyo kuelezea maendeleo ya Kampuni na uuzaji wa hisa unaoendelea hivi sasa nchini kote. Nawaombeni wote tuweze kuhudhuria tupate taarifa ya maendeleo ya *NICOL* na pia wale ambao hawajajiunga kwa kupata hisa, basi itakuwa ni fursa ya kuweza kununua hisa katika Kampuni hii ambayo ni kama Kampuni mama ya Uwekezaji kwa ajili ya wazalendo.

Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli anaye mgeni wake ambaye ni Bwana H. Omar - Afisa Tarafa, Tarafa ya Bumbuli katika Jimbo la Bumbuli. Yule pale! Karibuni sana.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anao wageni wake kama ifuatavyo: Ndugu Samson Katalama - Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera; yule pale *Speaker's Gallery*; ndugu D. K. Mtabalike Mkuu wa Wilaya ya Muleba, yule pale; ndugu Christopher Kulanja Katibu wa Uchumi na Fedha CCM Muleba; naona mtando wa Mheshimiwa Stephen Wasira ni mrefu kidogo mpaka Mkoa wa Kagera toka Mara. Kwa hiyo, hawa ni marafiki zake. Karibuni sana Viongozi wa Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni taarifa za Mikutano na Vikao. Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangizia Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 11 Aprili, 2008 saa 5.30 kutakuwa na mkutano wa Kamati hiyo ya Kilimo, Mifugo na Maji ukumbi Na. 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala.

Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Masuala ya UKIMWI wakutane saa 8.00 mchana leo katika ukumbi Na.231 ghorofa ya pili jengo la Utawala. Ni *briefing* fupi kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga - Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kwamba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wakutane leo tarehe 11 Aprili, 2008 saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Na. 432, yaani ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ameniomba nitangaze kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii wawepo kwenye Kikao saa 5.00 asubuhi leo katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani pengine wanakutana na wadau. Kwa hiyo, watakutana kwenye Ukumbi mkubwa wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Semina, napenda kuwakumbusha kwamba kesho asubuhi Jumamosi tarehe 12 Aprili, 2008 kutakuwepo na Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote na Semina hiyo inahusu Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Uhifadhi ya Jamii wa mwaka 2008. Semina itanza saa 3.00 asubuhi. Nawaomba mtunze muda ili tuweze kukamilisha shughuli zetu mapema. Semina hiyo imeandaliwa na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana - Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya. Itifaki zote zinazohusiana na Semina zimezingatiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kesho hiyo hiyo saa 8.00 mchana Shirika la *Mission Aviation Fellowship (MAF)* watakuwa na hafla ya kusherekea miaka 45 ya Shughuli ya Usafiri wa Anga kwa kutumia ndege nyepesi. Sherehe hizo zitafanyika kwa Anga lililopo Uwanja wa Ndege Mjini Dodoma. Mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Andrew Chenge.

Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa pale *Airport* kwenye Anga ya *MAF* saa 8.00 mchana katika hafla ambayo itakuwa na viburudisho na *briefing* kusherekea miaka 45 ya Shughuli za Usafiri wa Anga kwa kutumia ndege nyepesi hapa nchini.

Waheshimiwa Wabunge, jana haikuwezekana kuwa na Kikao chetu cha Kamati ya Kanuni. Kwa hiyo, napenda kuwatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba sasa leo hii saa 5.30 katika Ukumbi wa Spika kutakuwa Mkutano wa Kamati ya Kanuni.

Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni tafadhali wahudhurie bila kukosa ili tukamilishe suala muhimu linalohusu utaratibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu suala lililoletwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir juu ya *CD* ile ya *TANAPA* inayokuwa na matatizo kidogo kwenye maelezo ya kuhusu Muungano wetu. Nimearifiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Jumatatu ijayo Serikali itatoa maelezo ya Waziri na yatasaidia katika kueleza hali halisi ya jambo lenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi nimepata taarifa sasa hivi kwamba Mheshimiwa Balozi wa Ujerumani nchini Mheshimiwa Wolfgang Ringe ameingia humu na huyo hapo.

Mheshimiwa Wolfgang Ringe amekuwa muhimu sana katika kuimarisha katika miaka minne hii iliyopita uhusiano baina ya Tanzania na Ujerumani. Amefanya kazi nzuri sana, uhusiano wetu na Ujerumani ni imara na bila shaka nitapata nafasi ya kumshukuru zaidi mwezi Juni, 2008 ambapo atakuwa anatuaga kwa sababu atakuwa anamaliza muda wake.

*Thanks very much Ambassador Ringe, we are very much honoured by your presence but also the fact that you have been instrumental in enhancing very cordial relationship between Tanzania and Federal Republic of German. Ahsante sana.*

Waheshimiwa Wabunge, nitaongoza Ujumbe wa Mkutano wa Mabunge ya Dunia *Weekend* hii kwenda *Cape Town* na wafuatao ndiyo Ujumbe wangu. Mheshimiwa Kilonsi Mporogomyi, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Susan Lyimo.

Waheshimiwa Wabunge, mimi binafsi nitarejea wiki ijayo kwa ajili ya Shughuli za Bunge, lakini wenzangu wataendelea kidogo na kikubwa kilichopo ni kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa kumchagua Rais wa Umoja wa Mabunge ya Dunia na nchi za Afrika tumekubaliana kwamba Spika wa Namibia ndiye mgombea wetu. Kwa hiyo, inabidi kwenda kumpa kwa Kiswahili cha sasa hivi kwenda kumpa tafu.

Kwa hiyo, hilo mtuombee ili tuweze kufanikisha. Lakini uchaguzi wenyewe ni mwezi Oktoba, 2008 katika Mkutano mwingine, lakini maandalizi ni haya ya sasa, kwa sababu amechomoza mgombea mwingine kutoka Bara la Asia. Kwa hiyo, inatubidi tukaweke nguvu kidogo. Huo ndiyo mwisho wa matangazo.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (*The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Ndani na Nje Nchi, yaani *the Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008* pamoja na orodha ya marekebisho iliyosambazwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kutoa pole kwa wananchi wa Manyara na wananchi wote wa Tanzania walioguswa kwa namna moja au nyingine na



tukio la kusikitisha la maafa yaliyotokea katika mgodi wa wachimbaji wadogo wadogo katika eneo la Mererani.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niipe pole familia ya Askari wangu, Askari Na. A8971 - Koplo Athumani Hassan Mkomba aliyefariki dunia katika ajali ya maji akiwa akisafirisha gari la Magereza kuelekea Mafia kwa kutumia meli ya *MV Hobasi* siku ya tarehe 6 Aprili, 2008. Aidha, niwape pole Watanzania wote kwa ujumla wao waliokumbwa na maafa ya aina mbalimbali. Tukubali tu kwa imani kuwa yote hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja ndani ya Bunge lako Tukufu, toka niteuliwe na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ningependa kutoa shukrani zangu za dhata kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniteua na kuniamini. Kwa kupitia kwako na Bunge lako Tukufu, naahidi kwamba nitafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu kwa ajili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa shukrani zangu za pekee kwa mzee wangu Joseph James Mungai, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kwa kunilea na kunifundisha kazi nilipokuwa Naibu Waziri wake katika iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru pia waliokuwa Mawaziri katika Wizara ya Usalama wa Raia Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kwa kuanza kuibua mjadala wa suala hili na hatimaye Serikali kuona haja ya kuwa na Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nitamsahau Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki - Mbunge wa Bukoba Mjini, amenisaidia sana kwa kuwasilisha kwa umahiri Muswada huu mbele ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Niishukuru pia Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Bunge chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi - Mbunge wa Muleba Kusini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mussa Azan Zungu - Mbunge wa Ilala kwa kuupitia na kuuchambua Muswada na kuangalia maeneo ya kufanyia marekebisha ambayo yamezingatiwa na Wizara yangu. Wajumbe wa Kamati hiyo wanao uzoefu mkubwa sana, wamekuwa msaada mkubwa kwangu niliye mpya katika Sekta hii. Ninawashukuru sana.

Ninayashukuru Mashirika ya *National Organization for Legal Assistance (NOLA)*, *Legal and Human Rights Centre (LRC)* na *Tanganyika Law Society (TLS)*, bila kuwasahau Waandishi wa Habari kwa michango yao mizuri ya kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuongelea Muswada ambao upo mbele yetu siku ya leo, naomba nichukue fursa hii kutoa pongezi kwa ndugu Benedict Ngalama Ole-

Nangoro kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Muswada huu ni Azimio la Umoja wa Mataifa dhidi ya uhalifu wa Kimataifa lililopitishwa kwenye Mkutano uliofanyika Palomo Italy mnamo tarehe 12 -15 Desemba, 2000 ambapo Tanzania ilikuwa ni miongoni mwa nchi zilizoshiriki Mkutano huo na kukubali kutia saina Mkataba dhidi ya uhalifu wa Kimataifa pamoja na Itifaki zake. Mojawapo ya Itafiki hizo ni Itafiki inayokatiza usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto iliyotolewa na Mkutano wa Palomo pia upungufu uliopo kwenye Sheria zetu za sasa ambazo hazina wigo mpana wa kushughulikia makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu ndani na nje ya nchi ndiyo umetufanya tulete Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutunga sheria hii ni kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu nje na ndani ya nchi. Biashara hii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka duniani kote. Biashara huendeshwa kwa njia mbalimbali kama vile ulaghai, kurubuni pia kutumia nguvu kunakofanywa na wahalifu ambao nia yao ni kutunufaisha na biashara hii haramu. Tafsiri sahihi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu hususan watoto, wanawake na ni lazima mambo manne yafuatayo yadhahirike. Kuwapata, kuwasafirisha, kuwahifadhi na kuwatumikisha waathirika hao, yaani *Recruitment, Transportation, Harboursing and Exploitation*.

Mheshimiwa Spika, vipo viashiria vinavyoonyesha kwamba biashara hii ipo hapa nchini. Pamoja na kwamba sio kwa kiwango kikubwa ni msimamo wa Serikali kwamba hata hicho kiwango kidogo ambacho kipo lazima kidhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Muswada huu wadau wafuatao wameshirikishwa. Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), *Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)*; *Kihota Women Health and Development Organisation (KIWOHEDE)* na wote wameafiki juu ya umuhimu wa kutungwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kutungwa kwa sheria hii ni kama ifuatavyo: Itasaidia kuimarisha udhibiti wa uhalifu huu wa kimataifa wa usafirishaji haramu wa binadamu, tutapata fursa ya kushirikiana na Jumuiya mbalimbali za kimataifa katika kubadilishana taarifa zinazohusiana na wanaofanya biashara hii haramu. Baadhi ya sheria zitarekebisha ili ziendane na matakwa ya sheria hii ikiwa ni pamoja na kifungu cha 139(a)(1) cha Sheria ya Jinai (*The Penal Code*) na Watanzania hawatateseka ndani na nje ya nchi kwa kutumikishwa kazi kama watumwa bila malipo au kwa ujira mdogo kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusu sheria hii ni muhimu. Elimu hiyo itatolewa kupitia vyombo vya habari vya TV, Redio na magazeti, vipeperushi, matangazo, majarida na mabango. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa watumishi wa Taasisi ambazo ni muhimu katika kupiga vita biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu kutokana na ongezeko la vitendo vinavyohusiana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu hapa nchini na duniani kote jambo linalohitaji kuwa la sheria la kudhibiti biashara hiyo. Kwa mantiki hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipitia Muswada, Kamati ilitoa mapendekezo ya kufanya marekebisho katika ibara kadhaa za Muswada. Baada ya kuyatafakari mapendekezo ya Kamati Serikali imekubali kufanya marekebisho katika baadhi ya ibara za Muswada kama ilivyoainishwa jedwali la marekebisho ambalo limegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu umegawanyika katika sehemu kuu nane kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza ya Muswada yenye kifungu cha kwanza hadi cha tatu, inapendekeza mambo ya utangulizi ambayo ni jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno na msamiati muhimu inayotumika katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 2 yenye kifungu cha nne hadi cha nane inapendekeza masharti yanayoainisha makosa ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Sehemu ya tatu yenye kifungu cha tisa hadi 17 inapendekeza kuweka utaratibu wa upelelezi na uendeshaji wa kesi zinazohusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne yenye kifungu cha 18 hadi 25 inahusu masuala ya uokoaji, urekebishaji, ulinzi, ushauri nasaha na misaada inayoweza kutolewa kwa waathirika wa biashara hii haramu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano yenye kifungu cha 26 hadi 30 inahusu uanzishwaji wa mfuko utakaoshughulikia kupiga vita biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Sehemu ya sita yenye kifungu cha 31 hadi 34 inapendekeza uanzishwaji wa Kamati ya Kupiga Vita Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu na imeainisha muundo na majukumu ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba yenye kifungu cha 35 hadi 38 inapendekeza masuala mchanganyiko. Masuala hayo yanajumuisha ulinzi wa kisheria kwa waathirika wa biashara hii haramu, matumizi ya sheria nyinginezo na kanuni. Sehemu ya nane yenye kifungu cha 39 hadi 42 na ya mwisho inapendekeza marekebisho ya vifungu vya baadhi ya sheria ili kuiwezesha sheria inayopendekezwa kutungwa kufanya kazi kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa kutoa maelezo ya Muswada huu. Kupitia kwako, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waupitische na nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuwasilisha hoja hiyo ambayo imeungwa mkono. Sasa ni zamu ya Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili tupate maoni ya Kamati hiyo.

**MHE. JUMA S. KILLIMBAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008, yaani *The Anti-Trafficking in persons Bill, 2008* kwa mujibu wa Kanuni ya 115 (2) ikisomwa pamoja na nyongeza ya sita 8 (4) na 9(1) (b) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikaa tarehe 03 Aprili, 2008 hadi tarehe 04 Aprili, 2008 ili kuupitia na kuuchambua Muswada ikiwa ni pamoja na kuwasikiliza wadau. Kamati ilielezwa kuwa Muswada huu kwa ujumla wake unakusudia kutekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa dhidi ya uhalifu wa Kimataifa pamoja na itifaki ya Umoja wa Mataifa ya kuzuia, kukataza na kuadhibu usafirishaji haramu wa binadamu hususan wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa kina kuhusu Tanzania kuridhia Azimio hili la Umoja wa Mataifa pamoja na Itifaki ya Umoja wa Mataifa, ulitolewa na Mheshimiwa Balozi Hamisi S. Kagasheki - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati akiwasilisha Muswada huo mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Kamati kuzama katika uchambuzi wa kina wa Muswada huu kifungu kwa kifungu, tulipata nafasi ya kuwasikiliza wadau waliofika mbele ya Kamati. Wadau hao waliwakilisha Taasisi za *National Organization for Legal Assistance (NOLA)*, *Legal and Human Rights Centre (LHRC)* na *Tanganyika Law Society*. Wadau hao walitoa mchango mkubwa sana kwa Kamati na kuwawezesha

Wajumbe kusaidia katika kuuboresha Muswada huu. Muswada huu unapendekeza masharti mbalimbali kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ikiwa ni pamoja na utaratibu wa upelelezi na uendeshaji wa kesi zinazohusu biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu, masuala ya uokoaji, urekebishaji, ushauri na misaada inayoweza kutolewa kwa waathirika wa biashara hii pamoja na uanzishaji na uendeshaji wa mfuko unaoshughulikia mapambano dhidi ya biashara hiyo. Mengine ni uanzishaji wa Kikosi cha Kazi cha Kupambana na Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu na marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuiwezesha sheria kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuuleta Muswada huu ambao licha ya kuwa unajitosheleza, bali pia umezingatia mambo mengi muhimu katika kuzuia, kukataza, kudhibiti na kupambana na tatizo hili ambalo linakuwa kwa kasi duniani. Pamoja na hivyo Kamati ilipopitia na kuuchambua Muswada huu ilikuwa na maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo mengine ya Muswada kuzingatia mambo muhimu, Kamati ilikuwa na maoni kadhaa juu ya lugha na matumizi ya baadhi ya maneno katika Muswada huu. Mojawapo ya maeneo ambayo Kamati ilikuwa na maoni tofauti na maneno yaliyotumika kwenye Muswada huu ni kifungu cha nne ambapo Kamati inapendekeza kuwa yatumike maneno “*in persons*” badala ya “*in person*” ili kuleta mantiki iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 8(g) maneno “*trafficking person*” yametumika na kuharibu madhumuni ya kifungu hicho. Kamati ilipendekeza kuwa badala ya neno “*trafficking*” litumike neno “*trafficked*” ili kumlenga mtu anayesafirishwa na kuleta mtiririko mzuri wa kimaudhui.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu matumizi ya maneno ya Kingereza “*may*” na “*shall*” yanabeba maana tofauti yanapotumika. Kamati ilizingatia umuhimu wa kuwa makini na matumizi ya maneno hayo ili kuipa sheria uzito unaofaa. Katika kifungu chote cha 15 neno “*may*” limetumika kueleza utoaji wa fidia kwa muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, jambo ambalo linaonyesha kuwa sheria inayopendekezwa hailazimishi muathirika wa biashara hiyo haramu kulipwa fidia. Ni maoni ya Kamati hii kuwa fidia kwa muathirika katika kosa la usafirishaji haramu inapaswa kuwa jambo la lazima. Busara za Mahakama zipewe nafasi katika kuamuru kiasi cha fidia na ulipaji wake. Kwa hiyo, Kamati imependekeza kuwa badala ya neno “*may*” sasa litumike neno “*shall*” katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7(1) kinamtaja mtu anayesaidia usafirishaji haramu wa binadamu kuwa anafanya kosa la jinai. Aidha, kifungu kidogo cha (2) (a) kinatoa tafsiri ya mtu huyo kuwa ni yule anayeshiriki au kujihusisha na masuala ya usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa namna kifungu hicho kilivyo, mtu atakayehusika na usafirishaji haramu wa binadamu hata kama ni kwa kutokujua atakuwa hatiani. Ili kuuboresha eneo hili, ni maoni ya Kamati yangu kuwa neno “*knowingly*” linapaswa kuongezwa katika kifungu kidogo cha 2 (a) baina ya maneno “*who*” na “*participates*”

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 (4) kinataja kuwa jina la maelezo juu ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu au mtuhumiwa havitadhihirishwa kwa Umma. Kwa kuweka maneno “*or of the accused*” Muswada utakuwa unapendekeza kuhifadhiwa kwa jina la Mtuhumiwa hata pasipo ulazima wa kufanya hivyo. Kamati inapendekeza kuwa kifungu cha maneno “*or of the accused*” kiondolewe katika sehemu hii.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kisarufi ambalo ni muhimu sana kwa tafsiri ya sheria, Kamati ilipopitia kifungu cha 35(1) iliona kuwa maneno “*A trafficked persons*” yana makosa ya kisarufi, hivyo Kamati ilipendekeza kuwa neno ‘A’ kabla ya “*trafficked persons*” liondolewe na kubaki “*trafficked persons*”.

Mheshimiwa Spika, katika suala la lugha, Kamati pia inaona kuwa kifungu cha 6(3)(a) kinaainisha usafirishaji haramu wa binadamu pale ambapo umefanywa na kundi la watu watatu au zaidi. Ni maoni ya Kamati hii kuwa neno “*three*” libadilishwe na kuwa “*two*”.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni ya Kamati yangu juu ya matumizi ya lugha katika Muswada huu, vile vile Kamati ina mapendekezo katika maeneo mengine kama vile mambo yaliyotajwa kuwa ni usafirishaji haramu wa binadamu, msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (*DPP*) na Kamati ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la watumishi wa ndani nchini Tanzania limekuwa ni tatizo, ni maoni ya Kamati hii kuwa kifungu cha 4(a) hakitoi uzito unaotakiwa kuhusu tatizo la watumishi wa Ndani. Kamati inapendekeza kuwa ili kuwatendea haki wafanyakazi wa ndani na waajiri wao ambao wana uhusiano ulio halali, sheria lazima ifanue zaidi na kubainisha ni wakati gani utumishi wa ndani (*Domestic labour*) unakuwa usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6(2) kinabainisha mambo ambayo yanafanya usafirishaji haramu wa binadamu utambulike kuwa tatizo na kosa zito sana. Kamati inapendekeza kuwa katika kifungu 6(2)(d) yaongezwe maneno “*or religions practitioner*” ili uhusika wa viongozi wa dini kwenye biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu liwe nalo ni miongoni mwa makosa mazito ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu huathirika kisaikolojia, kuna haja ya sheria inayopendekezwa kulizingatia hili. Katika kifungu cha 11 (2)(a) orodha ya msaada anaoweza kuupata mtu aliyeathiriwa na usafirishaji haramu wa binadamu haionyeshi kama mwathirika huyo anaweza kupata huduma ya kisaikolojia, yaani “*psychological treatment.*” Kamati inapendekeza kuwa katika fasili ya 2(a) ya kifungu cha 11 baada ya maneno “*medical treatment*” yaongezeke maneno “*and/or psychological treatment.*”

Mheshimiwa Spika, Muswada huu katika kifungu cha 16 unapendekeza kuwa kesi ya usafirishaji haramu wa binadamu itafunguliwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka Nchini (*DPP*). Katika kutafakari hili, Kamati ina maoni kuwa kifungu hicho kinamwongezea madaraka Mkurugenzi wa Mashitaka Nchini bila ya sababu, jambo ambalo linaweza kusababisha kuchelewa, kukwama na hata kufutwa kwa kesi kutokana na kanuni ya “*nolle prosequi*”, yaani uwezo wa *DPP* kuondosha kesi Mahakamani.

Kwa kuwa usafirishaji haramu wa binadamu ni kosa la jinai, uendeshaji wa kesi za namna hiyo utategemea sana ushahidi utakaotolewa Mahakamani. Kamati haioni haja ya kibali cha *DPP* katika kufungua kesi ya usafirishaji haramu wa binadamu. Kamati inapendekeza kuwa kifungu cha 16 cha Muswada huu kiondolewe.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati yangu pia yanagusa kifungu cha 24 cha Muswada ambacho kinahusu kuwarudisha waathirika wa usafirishaji haramu katika nchi zao. Fasili ya (2) ya kifungu hicho inaruhusu kutomrudisha mwathirika huyu nchini kwake au kutompeleka nchi nyingine pale ambapo kuna mazingira yanayoonyesha kuwa kufanya hivyo kunahatarisha maisha yake au ya familia yake.

Katika eneo hili pamoja na kuzingatia usalama wa maisha ya muathirika na maisha ya familia ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, Kamati imeona kuwa Muswada huu haupendekezi itakavyokuwa hadhi ya mwathirika wa aina hiyo endapo hataondolewa nchini. Tunajiuliza, mtu huyu atakuwa mkimbizi, atapata uraia au atakuwa mkazi asiye na ukomo wa ukazi wake nchini (*a resident with unlimited stay*). Baada ya majadiliano marefu, wajumbe walipendekeza kuwa Muswada huu ufafanue zaidi hadhi ya muathirika katika mazingira hayo, lakini pia kwa kuzingatia Sheria ya Uhamiaji ile ya Ukimbizi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililojitokeza katika Muswada huu ni muundo wa Kamati ya Kuzuia Usafirisha Haramu wa Binadamu.

Kifungu cha 31(2) kinaanzisha Sekretarieti kwa ajili ya kuishauri Kamati ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu inayoanzishwa chini ya kifungu hicho hicho na kifungu cha 32 na kile cha 33. Hata hivyo Muswada haufafanui hadhi ya Sekretarieti kama itajitegemea (*autonomous*) au itakuwa chini ya Wizara. Kamati inapendekeza kuwa kuna haja ya kubainisha hadhi ya Sekretarieti itakayoanzishwa chini ya kifungu cha 31(2).

Aidha, Kamati inapendekeza kuwa katika kifungu 32(2)f neno “*three*” libadilike na kuwa “*four*” ili Kamishna wa Magereza naye aongezwe kwenye Kamati. Sambamba na mapendekezo hayo, mamlaka ya uteuzi wa Kamati hiyo ipewe nafasi mbili zaidi ya kuteua watu wasiokuwa kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ili nitoe maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Aidha, namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Laurence Masha na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Balozi Hamisi S. Kagesheki kwa ushirikiano wa kutosha walioutoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Napenda pia niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa michango yao ya kina iliyoweza kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwililo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila na Mheshimiwa Edward N. Lowassa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dkt John, S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst Feteh S. Mgeni Mheshimiwa Ali A. Mohammed, Mheshimiwa Dkt Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen (Mst) Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Magalle J. Shubuda na Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu. (*Makofi*)

Pia niweze kumalizia kuipongeza Sekretarieti yetu iliyokuwa chini ya Katibu Athuman Hussein na Neema Kiula.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Killimbah ukimwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangaza awali, nalazimika kwenda kuongoza kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge na kwa hiyo nitamwita Mwenyekiti Job Ndugai ili aweze kuendeleza shughuli zinazofuata.

Niseme tu kabla yeye hajafika hapa kwamba, wachangiaji bado ni watatu tu na Muswada huu ni mzito kwa sababu tatizo hili ni kubwa. Ninao Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Kwa hiyo, nafasi bado ipo ya wengine wote wanaotaka kuchangia Muswada huu ili kuweza kuurutubisha na Serikali iweze kupata maoni ambayo yataboresha zaidi Muswada. Kwa hiyo, mnaendelea kukaribishwa.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*



**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, naomba nimwite anayewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MSEMaji WA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kwa kuweza kuwa hapa ili kutekeleza moja ya majukumu yangu niliyotumwa na wananchi wa Tanzania.

Pili, ntoa shukrani zangu kwako kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 kwa mujibu wa Kanuni 53(6)(c) na 86(6) Toleo la 2007 la Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ntoa pole kwa wale wote waliopona kutokana na janga la maji kujaa kwenye migodi ya Mererani.

Aidha, ntoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa, familia pamoja na wananchi wote wa Mkoa wa Manyara na Kilimanjaro. Sambamba na hilo ntoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Mwakyembe pamoja na wananchi wote wa Wilaya ya Kyela kwa mafuriko makubwa yanayoendelea katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza kwenye Muswada uliowasilishwa mbele ya Bunge hili napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi walioifanya katika kufanikisha uwepo wa Muswada huu. Japokuwa umechelewa kwa kuangalia matukio yanayotokea kusafirisha watoto kwenda nje ya nchi kwa ahadi ya kuwapatia maisha mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5 (5) kinachohusu adhabu inayotolewa kwa mtu yoyote ambaye atatenda kosa kwenye kifungu cha nne, Kambi ya Upinzani inaona adhabu zitakazotolewa katika kifungu hiki ziendelee na kifungu cha uharibifu zierendane na uharibifu uliofanywa kwa mhusika.

Hivyo basi, kifungu hiki kisimnyime Hakim au Jaji uwezo wa kutoa adhabu kali zaidi kwa mtenda kosa kwa kulingana na kifungu cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tano na sita vinahusu adhabu kwa matendo ya kusaidia usafirishaji haramu wa binadamu na kukithiri kwa usafirishaji haramu kama ambavyo tulivyopendekeza hapo juu kuwa adhabu ziangalie kiwango cha uharibifu uliotokewa kwa mhusika. Ila Kambi ya Upinzani inaongezea kuwa kama makosa hayo yanafanywa na Kampuni faini ziongezwe na Wakurugenzi wa Kampuni husika wakabiliwe na kifungu gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9(2) kimetumia neno “*organs*” lakini kwenye tafsiri ya maneno neno “*organs*” kimetolewa tafsiri ambayo haitoi maana iliyokusudiwa katika kifungu hicho cha 9(2). Kambi ya Upinzani inaona itakuwa vyema tafsiri ya neno hilo liongezwe ili isije ikatoa mwanya kwa watu kutumia vibaya tafsiri hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18(2) kinachosema kuwa, “Mwathirika wa biashara haramu ili kurudi katika hali yake ya kawaida akawekwa chini ya uangalizi wa Afisa wa Ustawi wa Jamii”, Kambi ya Upinzani inaona ingekuwa ni bora kama lingeingezwa neno “*qualified*” kwani inawezekana kabisa Afisa Ustawi wa Jamii kutokuwa na taaluma ya kutosha katika kumhudumia muathirika na kushindwa kumfanya arudi katika hali yake ya kawaida kabla ya kuwa muathirika ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 kinachohusu vyanzo vya mapato kwa ajili ya uzalishaji wa Mfuko wa Kushughulikia Mapambano Dhidi ya Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu tunaona kuwa pamoja na vyanzo vyote vilivyoorodheshwa katika kifungu hicho pia faini zinazotolewa kwa wale wote wanaobainika kutenda makosa baada ya kulipa fidia kinachobaki kingewekwa kwenye kifungu hicho pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 32(1)(a) kinachohusu uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati kwamba atachaguliwa kutokana na watu wenye nyadhifa au waliokwishashika nyadhifa za ukamishna Mkuu wa Polisi, Uhamiaji na Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, Kambi ya Upinzani inaungana tena na wadau waliopendekeza kuwa nafasi hiyo ya Uwenyekiti wa kikosikazi kinahitaji mtu mwenye nguvu na sio yule aliyemaliza muda wake wa kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kabisa Tanzania bado ina watu wenye nguvu na sifa za kuongoza kikosi hicho badala ya wastaafu. Aidha, kifungu hicho kimetoa mwanya finyu katika uteuzi, hivyo basi, ni bora kuwepo na wigo mpana badala ya kujifunga kwa kutoa kigezo cha vyeo badala ya sifa kwa wale wote wanaotakiwa kuwemo katika mchakato wa kuteuliwa kushika nafasi hiyo ya Uenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada huu unaohusiana na masuala ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuanza kutoa pole kwa wale wote waliofariki na familia zao katika machimbo mbalimbali nchini, nikianza kule Mererani pamoja na machimbo ya Chunya, kule Mbeya. Vile vile nachukua nafasi hii kutoa pole kwa wale ambao walifariki kutokana na ajari za magari ambazo zimetokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wote nchini nichukue nafasi hii pia kuishukuru sana Serikali yetu kwa kuleta Muswada huu unaohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu. Ni kweli kwamba Muswada huu unawahusu watu wote nchini, ndiyo maana tunasema *trafficking in person*, lakini tuna hakika kabisa wahanga wakubwa wamekuwa ni wanawake. Baadhi ya maeneo

wanasafirishwa wenyewe na baadhi ya maeneo wanasafirishwa watoto wao na wao wamekuwa ni wazazi ambao wako mstari wa mbele sana.

Kwa hiyo, wanawake katika nchi yetu wamekuwa ni *victims* kwa sehemu kubwa sana na ndiyo maana siku zote tunajaribu kuwatetea sana wanawake. Tumekuwa na maazimio mbalimbali kwamba kundi hili katika nchini yaetu ni kundi kubwa. Zaidi ya asilimia 51 ya idadi ya watu wa Tanzania ni wanawake. Kwa hiyo, wanahitaji kuangaliwa sana. Ndiyo maana tunakuwa na *declarations* mbalimbali kuanzia Beijing hadi *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ndiyo maana tumekuwa tukiomba na kusisitiza sana kwamba wakati umefika wa wanawake na wanaume katika vyombo mbalimbali vya maamuzi kufikia asilimia 50 kwa 50. Niipongeze pia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu.

Naendelea kushauri kwamba, Muswada huu kwa maoni yangu usibaki tu Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu yapo baadhi ya maeneo ambayo yanatakiwa yahusiane na Wizara nyingine ikiwa ni pamoja na Wizara ya kazi na Maendeleo ya Vijana na Wizara nyingine. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Wizara kwamba ipo haja ya kushirikiana kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze kwa kuangalia Muswada huu. Nilikuwa naangalia lile eneo la tafsiri nikawa najaribu kuangalia maana ya neno 'Usafirishaji Haramu.' Ni kweli sehemu ya pili umeelezea ni matukio gani ambayo kwa tafsiri yatamaanisha usafirishaji haramu wa binadamu. Lakini naomba Wizara kupitia wataamu wake watoe *definition of the word 'Trafficking in Person'*. Tunahitaji tafsiri ya neno hilo na baada ya ile tafsiri tutakubaliana kwamba yapo matukio ambayo yata-*constitute* kutambulika kwamba ni *trafficking in person*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri hiyo itasaidia sana kwa sababu baadhi ya maeneo yapo mahitaji ya nguvukazi, kwa mfano eneo ambalo mimi natokea Mkoa wa Iringa, eneo ambalo wanalima sana miti na kupasua mbao, *Sao Hill* kule Mufindi. Maeneo yale wanahitaji sana nguvu kazi na Wilaya ile idadi ya watu haitoshelezi, hivyo huwa wana-*mobilize* watu kutoka maeneo mbalimbali na wakati mwingine watu wakifika pale wanalipwa kihalali na taratibu zinafanyika.

Sasa shughuli kama hizi tungependa zifahamike. Je, na hii nayo ni usafirishaji haramu wa watu kwenda maeneo yale ya kufanyia kazi kule ambako wanahitajika wafanyakazi wenye nguvukazi ya aina hiyo? Ndiyo maana nahitaji sana Serikali itusaidie tafsiri ya usafirishaji haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba Muswada huu utasaidia sana kulinda haki za binadamu. Katika nchi yetu tumekuwa na uhitaji sana wa sekta mbalimbali za kazi. Sekta hii ni pamoja na wale ambao wanafanya kazi majumbani, kwa lugha za wenzetu wanaita *domestic helpers*, jambo hili lipo na sote lazima tukubaliane.

Sasa ni wajibu wa Serikali kuangalia: Je, uhitaji wa kada hii ya nguvukazi inaandaliwaje na Serikali? Kama inafika wakati wasaidizi wa majumbani watapelekwa labda katika vyyuo maalum kwa mfano *VETA* na Serikali ikatamka kipato chao halali na sio hilo tu na sifa za watu ambao wanaruhusiwa kufanya kazi za majumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Muswada huu ni mwanzo mzuri ambao utasaidia sana kulinda haki za binadamu. Huko nyuma watoto wetu wengi sana katika Mikoa yetu yote 26 kutoka maeneo ya vijijini walikuwa wanachukuliwa kufanya kazi za majumbani na wanapokwenda kufanya kazi za majumbani wengine wanafanya kazi za mifugo na wengine za uvuvi wakati mwingine haki yao ya kupata elimu ya msingi (*compulsory education to all*) kutoka darasa la kwanza hadi la saba imekuwa ikikiukwa. Ilikuwa inategemeana tu na wadau mbalimbali katika jamii kuzingatia jambo hilo.

Kwa hiyo, bila shaka Muswada huu utakuwa ni mwanzo mzuri wa kuangalia maeneo hayo na kudhibiti. Baadhi ya maeneo wakati nafanya utafiti wangu mdogo watu walipokuwa wakiulizwa kwamba inakuaje watoto wanachukuliwa wengi maeneo ya vijijini kwenda mijini Dar es Salaam na Mikoa mingine kwenda kufanya kazi wanasema hatuna sheria ya kuzuia huo usaifirishaji.

Kuna nchi kama Indonesia wakati wanapeleka ripoti yao ya masuala ya haki za binadamu katika Umoja wa Mataifa mwaka 2006 takwimu zilionyesha kwamba kuna usafirishaji mwingi sana wa binadamu ambao ni haramu. Walipopeleka tena ripoti yao mwaka 2007 takwimu zikawa zinazidi kuongezeka na walipoulizwa walijibu kwamba hawana Sheria ya kuzuia usafirishaji haramu. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Muswada huu wa Kuzuia Usafirishaji Haramu utatusaidia sana.

Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za makusudi za kuamua kufuta ada katika shule za msingi na kupunguza ada ya shule za sekondari kwa sababu kwa kufanya hivyo pamoja na Muswada huu utatusaidia kuhakikisha kwamba watoto wetu ambao wako katika Wilaya zetu zikiwa ni pamoja na Ludewa, Makete, Mufindi na Njombe sasa watakuwa na nafasi nzuri ya kwenda shule na yeyote ambaye atatumika katika kuwasafirisha iwe kwa shughuli mbalimbali, basi bila shaka Muswada huu utatumika kuwadhibiti kwamba utakuwa ni usafirishaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kifungu cha saba cha Muswada huu, inaelezea juu ya *interpretation* ya maneno mbalimbali. Mimi naomba kushauri kwamba tafsiri hiyo ni nzuri, lakini pale ilipokaa kifungu cha saba sio mahali pake, ingewekwa katika sehemu ya kwanza ya Muswada huu ambako ndiko kwenye maana kamili ya tafsiri mbalimbali ya maneno ambayo yanatumika katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 cha Muswada kinaelezea juu ya haki ya watu kulindwa ili wasafirishwe, yaani usafirishaji haramu. Kifungu kinaelezea juu ya *protection and assistance of victims* na kifungu hiki kimeelezea wajibu wa Waziri na haki ya mwananchi kulindwa. Sasa kama tunazungumzia kwamba yule mwathirika ambaye amesafirishwa atakuwa ana haki ya kulindwa kupitia Wizara ama kupitia Serikali, basi tukubaliane kwamba upande wa pili kunakuwa na wajibu. Kama upande mwingine una

*right the other side* kuna *duty*. Sasa kama upande mwingine kuna wajibu, kifungu cha 19(3) kinasema kwamba, naomba ninukuu:

“*Protection, rehabilitation, assistance and other services to rescue victim shall be offered.*” Lakini kinaelezea kwamba: “*Subject to availability of resources.*” Sasa tukishasema *subject to availability of resources* inawezekana kabisa kila siku tukapata udhuru kwamba *resources* hazitoshi ndiyo maana tumeshidwa kuwalinda. Sasa kama ni wajibu, ndiyo maana tumesema *shall*, lile neno “*subject to availability of resources*” naomba liwe *deleted* kwa maana ni *claw back clause*, itazuia utekelezaji wa ulinzi wa watu kuhusiana na Muswada huu. (*Makofi*)

Lakini vilevile ningeomba Muswada uzingatie wadau mbalimbali maana usafirishaji haramu una wadau wa aina nyingi sana, lakini huu Muswada haujawagusa sana wale. Kwa hiyo, tuangalie. Kuna wadau kama mashirika ya dini, *NGOs* na wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, hawa ni wadau muhimu sana.

Ukienda kifungu cha 32 ambacho kinaelezea Kamati ya kuzuia usafirishaji haramu kwamba kutakuwa na Kamati. Kwanza naomba nishauri kwamba, hizo Kamati za kuzuia usafirishaji haramu ziwepo katika Mikoa na Wilaya zetu zote maana tuna Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, waangalie wale watumishi wa ile ile Halmashauri, basi waweze ku-*form* Kamati za uzuiaji usafirishaji haramu. Kusiwepo na Kamati moja tu katika nchi ambayo inakaa Dar es Salaam. Lakini pia Wajumbe wa ile Kamati wote ambao wameelezwa katika Kifungu cha 32(1) Kutoka (a) mpaka (i) ni *intellectuals*, ni watu wenye *professions* mbalimbali. Wanasema kutakuwepo na mwakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Mwakilishi wa Polisi asiyepungua cheo cha ukamishna.

Sasa hili jambo ni la Watanzania wote. Tunahitaji *participatory approach* kwenye *development*, kwenye masuala mbalimbali, hivyo lazima kuwepo na wananchi wa kawaida, wazazi, anayetoka kwenye Serikali ya Mtaa, yule mama kabisa anayekaa Mtaani, ambaye anajua malezi ya watoto, ambaye anafahamu nini ni vikwazo katika jamii; kama tatizo ni ajira ataweza kutoa *input* katika hiyo Kamati. Kwa hiyo, nashauri baada ya (k) (i) iongezeke (m) kuwepo na mjumbe ambaye ni *normal civilian personnel* na naomba sana awe ni mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, naona na muda wangu unakimbia, ningeomba sana, tumezungumzia juu ya usafirishaji haramu lakini ni muhimu sana Wizara ikaangalia sababu zinazopelekea usafirishaji haramu. Kama sababu ni kutokuwepo kwa ajira, basi tuangalie. Baadhi ya maeneo wanasema kwamba watu wanasafirishwa kwenda kwenye *centres* mbalimbali kutafuta ajira: Je, inakuaje kule anakotoka! Hizo ajira hazipatikani! Maana hii ni njia moja ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

Sasa hivi hadi nchi zinazoendelea unakuta watu wanatoka nchi zinazoendelea kwenda kwenye *developed countries* kwa mfano Uingereza kwa sababu kuna *cheap labour*. Anavyokwenda *foreigner* anaweza akalipa *four pounds per hour* lakini

Mwingereza anataka *ten pounds per hour*. Kwa hiyo, panakuwa na *migration of labour* kutoka kwenye nchi zinazoendelea kwenda kwenye nchi zilizoendelea.

Sasa ili kuzuia huu usafirishaji haramu ni muhimu sana tuka-*deal* na sababu zinazopelekea kwa watu kusafirishwa ni nini? Kama sababu ni vyanzo vya mapato, basi ni jukumu la Serikali na wadau mbalimbali kuangalia na kubuni vyanzo hivyo vikapata kwenye maeneo hayo husika. Kama ni maeneo ya Wilaya zetu, tuangalie! Kama ni kilimo, tunakiboresha vipi? Kama watu wanalima, tatizo ni masoko, basi hayo masoko yapatikane ili watu wasiweze kusafirishwa kwenda kwenye maeneo mengine ambako kwa imani yale maeneo mengine upatikanaji wa pesa au vyanzo vya mapato unapatikana kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada huu muhimu kwa Taifa letu. Naomba pia nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako na Wabunge wote kwa kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili. Nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kwa msiba mkubwa walioupata katika machimbo ya Mererani na naomba pia nimpe pole Mheshimiwa Mwakyembe kwa Jimbo lake kukumbwa na mafuriko makubwa kwa wananchi wa Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kuunga mkono Muswada huu mia kwa mia na niwashukuru sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuuleta Muswada huu ambao tulikuwa tunaubiri kwa muda mrefu. Biashara haramu ya usafirishaji wa watu hasa tukilenga watu wanaozungumziwa asilimia kubwa ni wanawake na watoto. Ni tatizo kubwa sana duniani, hasa Tanzania tatizo hili linakuwa kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, Muswada huu tunauhitaji na mimi nafikiri wananchi wote wanatakiwa waelemishwe waweze kuuelewa Muswada huu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu tunaelewa kwamba vijijini mwetu watoto na hasa watoto wa kike wanasafirishwa na kwa wakati mwingine wanasafirishwa kwa ajili ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kwamba hili ni tatizo na mara nyingi huwa wanadanganywa na wale watu wanaokuja kuwachukua watoto kwa kuwaahidi ajira kubwa na wakati mwingine kuwaahidi hata kusoma, hasa kwa wale wanaopenda elimu wakijua kwamba mtoto anapenda elimu, basi wakimwambia tukikuchukua unakwenda kupata elimu na vivutio mbalimbali ambavyo wanakuwa wanaviahidi. Kinyume chake wakishachukuliwa hao watoto wanatumikishwa, wanafanyishwa vitendo ambavyo ni vya kikatili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo hivi vimekuwepo hapa nchini kwa muda mrefu na wakati mwingine ilikuwa ni vigumu kuweza kuwakamata wahusika kwa sababu

haikuwepo sheria ambayo ilikuwa inaweza kutumika ili kuweza kuwabana. Kwa hiyo, napenda kuungana na Wizara kwa kuweza kuleta huu Muswada.

Lakini pia napenda kusisitiza kwamba baada ya Muswada huu kupita kuwa Sheria, elimu itolewe kwa wananchi huko vijijini na sheria yenyewe itafsiriwe kwa lugha rahisi ambayo itakuwa rahisi kwa kila mwananchi kuielewa. Ikibaki hii lugha iliyopo ya kiingereza ambayo sio rahisi mwananchi kuelewa, hata kama ni Kiswahili, basi kiwe Kiswahili rahisi. Itengenezewe muhtasari ambao mwananchi wa kawaida anaweza kuielewa hii sheria na kuweza kushiriki kikamilifu katika kuzuia tatizo hili na tatizo hili pia tunatakiwa tufanye utafiti na nina uhakika kwamba Wizara inaelewa kwamba huko vijijini sababu ziko nyingi zinazofanya watoto waweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sababu ndiyo tunatakiwa tujue chimbuko na tuanzia hapo kwamba kwanini wanasafirisha? Tukianza hapo, tunaweza kuzuia kuanzia ngazi ya chini. Nakumbuka zamani kulikuwa na utaratibu mzuri na naomba Wizara iliangalie; zamani kila mgeni aliyekuwa anakuja kijijini alikuwa anafahamika kwenye Serikali ya Kijiji au kwa Balozi. Lakini siku hizi watu wanakuja wanakaa vijijini huko na wanachukua watoto wanaondoka nao hakuna mtu anaweza kujua wamelala wapi. Mimi nafikiri huu utaratibu urudishwe. Naipongeza Wizara kwa kuanzisha Polisi Kata. Kwa kutumia Polisi Kata tunaweza kujua matatizo yanaanzia wapi na tunaweza kusema kwamba wananchi wote waweze kushirikishwa ili kuweza kutambua hili tatizo na kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba watoto wetu hawasafirishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kushauri ni kwamba tuangalie pia mipaka yetu tuwe na ushirikiano. Sina uhakika kwa nchi nyingine zinazotuzunguka kama nazo pia zinasheria kama hii. Tuna Afrika Mashariki, tuitumie hiyo nafasi ya nchi zinazotuzunguka kwa sababu tunajua kwamba wale wanaosafirishwa wanapita kwenye hizo nchi ili iweze kuwa rahisi kujua tatizo hili wanzetu nao wanalizua ili wasiweze watoto wetu wakapitishwa kwenye hizo nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia kipengele cha 21 kinachozungumzia watoto watakaokuwa wanafanyiwa *rehabilitation*. Ninafikiri mafunzo pia yaangaliwe, halafu wapewe vyanzo vya mapato na nina uhakika kwamba mfuko utakaoanzishwa utaweza kutoa vianzo vya mapato kwa sababu wengine wanachukuliwa kwa sababu ya kutokuwa na ajira na maisha duni ya vijijini na kwa maana hiyo kama watakuwa wamepewa vyanzo vya mapato ili waweze kujitegemea na kufanya shughuli ambazo wangependa kuzifanya. Kwa maana hiyo, napongeza taasisi mbalimbali hao watoto ikiwemo *KIWOHEDE* ambayo imeweza kufanya kazi kubwa ya kuweza kusaidia watoto hawa. Kwa hiyo, kwenye vituo huko wapewe mafunzo halafu kwa vile kuna watoto wengi wanaomaliza shule za msingi, elimu hii ianze kutolewa mashuleni, uingizwe mtaala wafundishwe ili wawe wanajua kabla hawajatoka shuleni.

Kwa sababu wengi wanaosafirishwa ni wale ambao wamemaliza darasa la saba, napenda kushauri kwamba Wizara ishirikiane na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Elimu ili kuhakikisha kwamba mafunzo haya yanaingizwa kwenye elimu ya msingi ili

watoto waweze kujua na pia wazazi na kamati za shule ziweze kupewa mafunzo. Pia nashauri kwamba tunaelewa kwamba kuna Wilaya nyingine zina Kamati za *Child Labour* za kuzuia ajira kwa watoto, napenda zioanishwe kamati hizi na nashauri kwamba Kamati isiishie kwenye ngazi ya Taifa tu, kuwepo na Kamati kwenye ngazi za chini kama tulivyo na Kamati nyingine ambazo zinaanza kwenye kitongoji kwenye mtaa zinapanda huko juu. Kwa sababu kila mahala kuna viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia *composition* ya Wajumbe wa hii Sekretarieti itakayoundwa, nimeona imegusa sana taaluma kama alivyosema Mheshimiwa Pindi na kugusa vyeo. Lakini suala la jinsia haijagusa, imesema Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, huyo mtu awe na cheo cha Mkurugenzi Msaidizi, haijasema ni nani, mwanaume au mwanamke na huko Zanzibar imesema hivyo hivyo. Kwa maana hiyo, hii Kamati imekuwa ni ya upande mmoja. Mimi nina wasiwasi tutakuta wamekaa watu wa jinsia moja na kwa kiasi kikubwa watakuwa wanaume wakati wale wanaohangaika na tatizo hili ni akinamama na watoto wao.

Napenda iandikwe kabisa kwamba katika Kamati hii itakuwepo idadi fulani ya wanawake watakaohusishwa na mimi ningeshauri kabisa, kama inawezekana tutaje kabisa hata hizo taasisi tunazofikiri zitaingia humo ziwe zile zinazojishughulisha na suala hilo na wale watu watakaolingia humo wawe ni wale watakaojishughulisha kabisa na suala hili. Kwa hiyo, mimi naomba suala la jinsia liangaliwe, wawepo wanawake na wanawake ambao wameguswa na tatizo hili na kwenye Kamati hizi zitakapokuwa zimeundwa pia kwenye ngazi za Wilaya ziangaliwe na iwe imeelezwa kama Kamati nyingine zinazoelezwa badala ya kufungwa tu bila ya kujua kwamba watakaokuwa humo wanaume watakuwa wangapi wanawake wangapi. Hilo nafikiri kwamba ni muhimu sana tuweze kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *domestic violence*, ninaelewa kwamba kuna sheria ya masuala ya kujamiiana, lakini naelewa pia kwamba tatizo la *domestic violence* ndiyo linalosababisha pia watoto kukimbia na inakuwa ni rahisi sana kuwachukua na kuwaambia kwamba nakwenda kukupa maisha bora. Kwa hiyo, na hilo napenda lioanishwe ili hii Sheria ioanishe na sheria nyingine zilizopo na vipengele vingine vya sheria pia viweze kufanyiwa marekebisho ikiwepo sheria ya ndoa, sheria ya masuala ya kujamiiana na sheria nyingine ambazo zina vipengele vinavyoweza kusababisha kuwepo na tatizo hili.

Baada ya kusema hayo naomba nirudie tena kushukuru na kuipongeza Wizara kwa kuweza kuleta Muswada huu muhimu na nina uhakika kwamba mafunzo yatatolewa sehemu mbalimbali ili Muswada uweze kueleweka, lakini wananchi pia waweze kushiriki kikamilifu katika kupambana na kukomesha usafirishaji wa watoto au usafirishaji wa binadamu. Sisi wengine tunaotoka kwenye mikoa ambayo imeathirika kwa watoto kuhama kutoka vijijini na kwa kuchukuliwa kwa kuahidiwa maisha bora na kupelekwa mijini ambako wanatumikishwa nina hakika kwamba suala hili litazingatiwa na sheria hii itakuwa imetusaidia kupunguza tatizo hili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo narudia tena kuunga mkono hoja ahsante. (*Mkofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ledaiana Mng'ong'o. Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokuwa mmeona wakati mkifuatilia mjadala huu wachangiaji wetu watatu wa mwanzo Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o wote wanatoka Iringa, nafikiri ni kwa sababu maalum kabisa, hivyo tunamtarajia Mheshimiwa Waziri atupe uhakikisho wa wananchi wa Iringa kuhusiana na masuala haya ya *trafficking in persons*.

Sasa twende Visiwani, naomba nimwite Mheshimiwa Haji Juma Sereweji - Mbunge wa Mwanakwerekwe atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Vilevile niipongeze hotuba ya Waziri ya Mambo wa Ndani ya Nchi na kutuletea Muswada huu. Lakini lazima tuelewe kwamba huu si Muswada wa viongozi wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu wa kwanza ni kwamba tutoe elimu kwa watanania wote kuwajulisha kwamba hivi sasa Tanzania imekumbwa na jambo hili. Lakini jingine tujiulize, kwa nini Tanzania imekumbwa na jambo kama hili ambalo vijana wetu wenye nguvu kazi wanaondoka? Lingine tujiulize, tutalizuiaje? Kwa nini limetokea na tutalizuia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna vijana wengi tu wenye umri wa miaka 17 mpaka 18 wanajitegemea wenyewe kimaisha na utawakuta wengine wamekwishakata tamaa na maisha, siyo kidogo! Lakini ukipita sehemu za Kariakoo hivi sasa kuna wavulana na wasichana kuanzia umri wa miaka 8, 10 hadi 15 wamekuwa omba omba. Ukiwatazama wale ni rahisi sana kurubuniwa, ama kuchukuliwa majumbani au kuondoshwa Tanzania na ndio maana nikajiuliza tuanze vipi, kwa nini na tutazuijae?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Muswada huu utatazama kwamba viongozi wa juu wote ndiyo wenye kamati na kumbe suala hili ni la wananchi vijijini, mitaani na kila sehemu. Kwa hiyo, natoa ushauri Muswada huu walengwa ni wenyewe wananchi wa Tanzania wote. Kamishna au Mkuu wa Polisi atafika fikaje Mtoni Mtongani na kuyajua ya Mtoni Mtongani?

Lakini atayajua vipi ya Mbagala au Iringa? Sasa hizi Kamati naomba ziwepo kila Mkoa na zianzie chini, lakini kuwe na elimu ya kuwaeleimisha vijana wetu hasara ambazo zitawapata baada ya kuondoka Tanzania na tuwaeleze kwamba huu ni utumwa baridi. Siku za utumwa binadamu walikuwa wanatunuliwa sehemu nyingine na kuuzwa na kupelekwa kwingine. Na kule wanakopelekwa wanatumiwa wanavyotaka wale watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala sisi tunasema linakuja kwa utaratibu, lakini mimi nasema linakuja kwa kasi kubwa sana kwa sababu wale walengwa ambao wanataka

kuondoshwa hapa au wanaondoshwa hapa, wao wenyewe watakuwa tayari baada ya kukata tamaa na maisha ya Tanzania. Sasa ombi langu ni kwamba Serikali jambo la kwanza kabisa itazame inaweza kulikabili vipi na kuwaandaa vipi vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalolisema mimi, sisi ndio tuliopo mitaani, tunayaona ya mitaani. Hivi sasa utapita sehemu ambazo ziko nzuri nzuri kabisa, lakini jioni wanapita watu wa Manispaa ambao utawakuta vijana wetu wanawekeza na kufanya biashara zao na kuanza kudhalilishwa. Hili nalo tungelitazama twende vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo leo nimepata nafasi ya kulizungumza kuhusu hawa wapambe wa Daladala, huwa najiuliza je, wenye Daladala wamekwishakubali kwamba wawe na wapiga debe huku wenyewe wakiwa wanatoa kwa kila mpiga debe shilingi mia? Lakini wakati huo huo wapiga debe wale wakiondoka pale wana kiasi cha shilingi 1000 mpaka 1500, lakini Serikali inasema wapiga debe wale wasiwepo na wako wengi sana, kwa sababu ni vibaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila kitu huwa kinaboreshwa. Ombi langu kutokana na mambo haya yanayojitokeza sasa hivi na wapiga debe wale huwa wanajisaidia wao pamoja na wazazi wao, waboreshewe maisha yao. Kama wachukuzi *customs* waorodheshwe, wawe na sheria zao na wawe na *uniform* ili wajulikane kuwa katika kila kituo pana wapiga debe vijana fulani, hata kama watalipa shilingi 3000 kwa mwaka. Sasa wale ambao watajitokeza kinyume na wale, hao ndio wa kubanwa. Hili ni ombi langu ninalileta kwa vijana na hasa kwa vile yanatokea mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye Kamati, Dar es Salaam alitokea mlemavu mmoja, yeye alieleza kwamba amechoka na hataki kuomba omba. Lakini akasema: “nimeweka biashara yangu hapa kila siku nasumbuliwa na leo nimekwishachukuliwa biashara yangu hapa mahali pazuri, basi bora nife.” Akajiweka chini ya gari ya Manispaa ili apondwe awe hayupo kabisa kabisa. Wakati mlemavu yule anafanya biashara ili aondokane na omba omba, sasa nadhani watu kama wale wa kufikiriwa na kutafutiwa sehemu. Na kama pale biashara yake inakwenda vizuri, patazamwe pamekaa vipi; je, anaweza kukaa au atafutiwe mahali pengine? Mlemavu wa miguu na mikono atafanya nini? Sasa hivi tumefikia wakati Watanzania hatujui tufanye nini kwa vijana wetu walio wengi kuliko sisi wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi tena kwamba Muswada huu ni wa wananchi wote vijijini. Kwa hiyo, kila Mkoa uwe na Kamati ya kuelimisha na kuwe na Kamati ya Ulinzi ya Mkoa ambayo ihusike na mambo haya ya kuzuia biashara haramu ya vijana wetu ambao wengine wanarubuniwa na wengine wanakwenda kwa hiari yao ili kubadilisha maisha sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Asante sana!  
(*Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi hii. Nilikuwa sitaki kuchangia lakini baada ya kuona watu kidogo, nikaona na

mimi nichangie. Kwanza kabisa, nakushukuru wewe kunipa nafasi. Lakini pili natoa pole kwa wenzetu ambao wamepata ajali kubwa kwa sababu ya mafuriko Mererani na Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kasema hili si tatizo kubwa nchini kwetu. Naomba kusema kama si tatizo kubwa, ni la miaka hii. Lakini miaka mitano/kumi iliyopita hili lilikuwa tatizo kubwa. Kuna familia nyingi zimeathirika kwa watoto wao kuchukuliwa na kusafirishwa katika suala zima tunalozungumzia la biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hujui uchungu wa wazazi waliokuwa nao Watanzania wengi nikiwa na mimi ni mmojawapo. Watoto walikuwa wanadanganywa wengi sana kwa kusema kuna maisha bora huko, kama siyo ndani ya Tanzania kutoka vijijini, kwenda nje ya Tanzania. Ndiyo maana watu wa Iringa wanazungumza kwa kweli kwa uchungu sana. Vijana hawa wakiletwa kwenda kufanya kazi huwa wengine wananyanyaswa na wengine wanalawitiwa na watu wanaowaajiri. Na wengine wamefikia hatua hata kuathirika kupata ugonjwa wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze hili kwa uchungu mkubwa na nashukuru sana Serikali na nasema kwanza naunga mkono mia kwa mia. Vijana wetu, akina mama wetu wanachukuliwa aidha na mashirika mbalimbali au waoaji na waolewaji au wafanyabiashara hasa biashara haramu, watu binafsi, *researchers* na waganga wa kienyeji. Tunalichukulia hili kwa urahisi. Mashirika mara nyingi yanawadanganya vijana wetu na kuwatumia watu binafsi kwa kusema kuna maisha bora huko ughaibuni. Vijana wetu wanaondoka lakini wakienda kule wananyanyasika. *Reseachers* wanawachukua vijana, ilizungumzwa Kenya na Tanzania ipo. Wanachukua vijana wakijidai watu wa dini, wanakwenda kule kuwafanyia *research*. Wengine wanawa-*adopt* lakini wanakwenda kuwafanyia *research*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati vita vya Iraq vilivyoanza, kwanza kabisa kule Ubalozi vijana wengi walikuwa wanakwenda wanasema kuna kazi. Lakini walichukuliwa vijana kwenda kupigana Iraq. Vita vya Somalia vilivyokuweco chini ya Jenerali Aideed, vijana wengi wa Kitanzania walichukuliwa wakaenda ikiwa ni pamoja na mtoto wangu, wakidanganywa kuna maisha bora. Wakifika kule wanaingia kupigana vita bila ya kutaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wanaambiwa twendeni *South Africa*. Kuna vijana wenzi wao wanakaa katika *jobless* wanasema *South Africa* kuzuri na kadhalika. Vijana hawa wanaosema *South Africa* kuzuri, waliandaliwa na watu binafsi na mashirika kuwadanganya vijana wetu waende *South Africa*, na kwingineko. Wakienda kule wanaishia kufanya kazi ya kuuza dawa za kulevyo na matokeo yao wanakuwa *addicted*. Kwa hiyo, si jambo la urahisi ilivyozungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijana wetu wengine wanatolewa vijijini kuletwa hapa kwa kuambiwa maisha bora, mwisho wanawekwa katika nyumba moja wanawake na wanaume kufanya kazi ya ngono, inasikitisha! Kuna baadhi ya vijana wanadanganywa kuwa wanakwenda kufanya kazi bora. Nakumbuka *instance* iliyotokea wakati kijana wa

kitanzania alipopelekwa Uganda, na kulikuwa na watu Uganda wanachukua watu hapa, wanakwenda kule, wanapelekwa wanakwenda kuuawa. Wanachukuliwa vitu, yaani miili yao na waganga hao wa kienyeji kwenda kufanya dawa za uganga. Nakumbuka kijana mmoja alipoona alikuja akaandika hata katika gazeti kwamba aliposikia wanazungumzia tayari kwa kumkata, kumchinja, aliweza kutoroka. Kwa hiyo, tunavyozungumzia *trafficking* si kitu cha urahisi rahisi watu wanachozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hii sheria isiishie tu kwa hiyo kamati ya watu wachache. Naomba sheria hii kwanza iandikwe kwa Kiswahili, wananchi washirikishwe katika kusimamia hili kwa sababu wao kweli ndio wanaoona, wanaoamia, ndio watoto na vijana wao waliochukuliwa. Mimi nakumbuka kabisa kuna mwenzangu mmoja alikuwa Mwanza, akadanganywa na Mzungu, akaolewa, akaenda zake, sitaki kusema nchi gani. Mpaka leo yule mama ameniletea picha na kusema jinsi anavyodhalilika. Yule mama amefika pale amezwa, amekwenda zake huko Ulaya, kafika pale akawa hawezi kurudi, viza halali hana, anateseka! Kwa hiyo, tunapozungumzia hili suala msifikiri rahisi rahisi. Na sehemu kubwa inasababishwa na hali ngumu ya maisha na mipango ya ajira haijakuwa kamilifu. Vijana wetu wananyanyasika, wanawake wananyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hizi kamati zianzie kwenye Serikali za Mitaa na Vijiji, kwenye Kata na Wilaya, Mkoa na Taifa. Hawa watawaambia. Hivi sasa hao vijana mnaowaambia wanaokuja kupiga debe walidanganywa, wakaja hapa, wanatumikishwa sasa hivi kuuza dawa za kulevya. Vijana wengi hawa *drug addict* tunawaita mateja, walitoka majumbani wakidanganywa. Anakuja hapa anaambiwa auze dawa, mwisho anaambiwa ili utake ku-*enjoy* dawa hii, ili uweze kuuza kama dawa hii ni vizuri, *ui-test, it will take you only five days*, uki-*test*, umekuwa *addict*, ndiyo vijana wetu wengi wameharibikiwa. Naomba hata hawa vijana, *drug addict* au mateja, wachukueni. *Symptoms* zinajulikana kwa *Psychiatrists*, watawasaidia kuwaonyesha hawa watu wanaojidai wafanyabiashara kumbe biashara zao haramu. Mimi naomba vijana hao wengine wako *ready* wanataka wasaidiwe, wameshindwa kuondoka katika *addiction*. Anataka aondoke, hana utaratibu, matokeo ile *addiction* inam-*force* aendeleo kula dawa zile, *otherwise* anaweza kupata *sudden death*. Kwa hiyo, naomba hili tusilichukulie kirahisi rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *psychological treatment*, mimi nafikiri hawa vijana ambao bahati nzuri walioathirika lakini wamerudi, naomba tuwasaidie kabisa tena tusiwasaidie kwa utani. *Psychologically they are affected*. Ninatoa mfano wangu mwenyewe binafsi kwa maana ya mtoto wangu. Alipelekwa, akapigana Somalia, bahati nzuri katoroka karudi, matokeo kijana yule akikaa anazungumzia, yaani aina yoyote ya silaha ikipigwa anakwamba hiyo ni silaha gani, silaha gani! Kijana yule hivi sasa naogopa, wakimuudhi tu, huwa hakubali, anapigana na akifikia kupigana anapiga kweli kweli! Imefika *stage* wanataka kumtumia mwenyewe yule mtoto kwa kumdhaliisha Dr. Gama.

Wamefikia *stage* wanamnyanyasa, wanajua ile hasira yake, sasa hivi imefikia hatua kijana yule alikwishaandaliwa hata kufungwa bila ya sababu, kwa sababu mtu

anamjua huyu ana hasira, hatumtaki mama Gama kwenye ubunge, kwa hiyo, tunataka mtoto wake aharibikiwe na sisi tumwandike. Wakamwingiza kwenye matatizo, kijana yule kweli uwezo wake wa kupiga anao, alipiga, matokeo wakambambikizia kesi, kesho yake wakamwambia aende mahakamani, akahukumiwa miaka miwili. Ningekosa mama yake mimi kuwa na uwezo na kuweka *Advocate*, yule mtoto angekwishahukumiwa miaka miwili bila kutoa ushahidi. Huyu mtoto ameathirika anatakiwa asaidiwe, matokeo anashindiliwa. Ndiyo maana nikasema elimu hii pia hata viongozi wetu pia wanayo, wanatakiwa waifanye, viongozi hata wa vyama, viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hawa vijana kwa kweli *they need psychological treatment* kuanzia hawa walioathirika dawa za kulevyu, hawa ambao wamechukuliwa ghafla ghafla wakaenda wakafanywa wanawake na wakanyanyaswa na wengine wakafanywa wanawake wakiwa wanaume, wakanyanyaswa na wengine imefikia hatua ndio hao nilikwambia *psychological*, hana la kufikiri, anafikiria bunduki na risasi. Naomba tuwasaidie, ama siyo wanatumiwa vijana hawa sasa kupoteza au kuvunja sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nashukuru sana. Nisingetaka kusema lakini ilibidi niseme nilivyoona watu wachache. Lakini wazazi wengi wanaumia. Nitatoa mfano, nilikwenda Mekka, nikaamua kuona. Wakati nikiwa katika Kamati ya Mambo ya Nje, nikaenda kwenye Ubalizi nikaambiwa kule Saudia Mashirika haya yanachukua watu kufanya kazi.

Vijana wetu wanaokwenda kupelekwa kufanya kazi za ndani, wananyang'anywa pasipoti, wanateswa, yaani mpaka wengine wanakufa, wengine wanakimbilia Ubalizi. Ubalizi hauna hela, inabidi tu uhangaika tu huku na huko. Naomba msifikirie jambo hili, ni *very serious* na vijana wetu na akinamama wetu wengi wanaathirika. Ahsante sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, nakushukuru sana na pole kwa yote! Sasa, nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu ambao kimsingi ni Muswada wa haki za binadamu. Jambo lolote linalohusu haki za binadamu ni suala ambalo lina misingi katika Katiba yetu ya nchi na dunia nzima inashughulikia suala la haki za binadamu kwa sababu wanadamu katika miaka ya nyuma wameonewa sana na ndiyo maana hata leo suala la haki za binadamu linatokea katika mada nyingi zinazohusu hata Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, natoa pole na pia rambi rambi kwa vijana wetu na wananchi ambao walipoteza maisha yao huko Mererani kwa sababu ya mashimo yao kutokuwa na teknolojia inayostahili. Pia ningependa kuwapa pole wananchi wa jimbo langu hasa wanaokaa maeneo ya mgodi kwamba sasa hivi watu zaidi ya mia wamekamatwa kwa sababu wanasingiziwa kwamba wanaiba dhahabu, wakati wao wanaona kwamba ndio wamevamiwa. Nadhani Serikali italiangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kwenda moja kwa moja katika suala la *trafficking*. *Trafficking* maana yake ni kumhamisha mtu kutoka eneo fulani kumpeleka katika eneo lingine kwa ajili ya kumtumia. Hapo kuna *definition* ambazo zimetolewa na naona tafsiri hizi ni pana sana. Kwa mfano, neno *abduction* ambalo ni kumlazimisha mtu au kwa kumteka, linazungumzia kwamba mtu anayekuwa kwa Kiingereza mmesema *abduction in relation to offences relating to trafficking in persons means to compel or induce a person to move from one place to another*. Hapo ndipo ambapo ningependa Serikali itusaidie ili tuone kama kweli hili neno *abduction* ambalo linahusiana na hii sheria ya *trafficking* limetafsiriwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumlazimisha mtu kutoka katika eneo fulani kwenda katika eneo lingine kwa ajili ya kumnyonya, kwa mfano wa biashara ya utumwa, kwa zaidi ya miaka 400 Afrika ilipata tabu kubwa ya watu wetu kuchukuliwa na inasemekana walichukuliwa watu zaidi ya milioni 600 na Tanzania ilikuwemo, watu wengi sana walichukuliwa kwenda katika utumwa kwa kulazimishwa. Lakini leo ukisimamisha magari sehemu au ndege ukiwauliza vijana wa Kitanzania kwamba: “ni nani ambaye anapenda aondoke hapa Tanzania aende utumwani?” Mimi nadhani utashaanga jinsi zile ndege zitakavyojaa kwa sababu nchi yetu sasa imekuwa ni sehemu ambayo Watanzania wenyewe kwa hiari yao wanaikimbia nchi hii ili angalau waende mahali popote hata akiwa mtumwa pale, lakini aweze kuishi maisha tofauti na haya anayoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inaonekana kwamba kumlazimisha mtu kutoka katika eneo moja kwenda lingine ni kwamba sisi wenyewe pia tunahusika kwa sababu kama vijiji vyetu ni maeneo ambapo wananchi hawataki kukaa sasa wanakimbilia mijini. Kwa hiyo, tunashiriki pia kuwalazimisha wananchi wetu kutoka hapa ndiyo maana vijana wetu wanaishia nchi zingine, Afrika Kusini, na kadhalika, wanaondoka wanakwenda. Wanatoka vijijini wanakwenda mijini, afadhali afanye umachinga au apige debe kuliko kukaa kule vijijini. Kwa hiyo, hiyo tafsiri iangaliwe na tuone kwamba sisi tunahusikaje kama Serikali kuwalazimisha watu kuingia katika masuala ya *trafficking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kuzungumzia ni kuhusu shule zetu. Shule zetu zinafanyisha watoto kazi kwa nguvu. Sasa je, hii ni *trafficking*? Maana anawatoa hapa, anawapeleka kwenye shamba la mtu au shamba lake, wanakwenda kufanyishwa kazi bila hiari yao. Je, hii inaingia pia katika *trafficking*? Kama ni hivyo pia ifafanuliwe hapa vizuri kwa sababu hiyo ni *slave labour*. Kwamba watoto hasa wa shule za *primary* wanashinda wakiwa wanafanya kazi kwenye mashamba ya watu hapa hapa nchini wakifanyishwa kazi na walimu.

Mimi naona hiyo pia ni *trafficking* na ni suala ambalo linatakiwa litungiwe sheria. Hata walimu wenyewe wanatolewa maeneo fulani wanapeleka maeneo mengine kufanya kazi ya ualimu halafu hawalipwi. Hiyo ni *trafficking* kwa sababu *definition* hiyo imeandikwa hapa bayana kabisa kwamba nini maana ya *trafficking*. Inasema *forced labour and slavery means the extraction of work or services from any person by means of incitement, enticement, violence, intimidation or threat, use of force or coercion including deprivation of freedom*. Sasa umempeleka kule kijijini hawezi kuondoka wala

hawezi kuacha kazi halafu humlipi. Hiyo ni *trafficking* pia lazima ielezwe hapa kwamba itachukuliwa hatua gani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kuzungumzia ni *trafficking* inayohusiana na majeshi. Katika ukurasa wa 6 part 3 inasema “*prohibition of trafficking of persons, acts of trafficking in persons.*” Inasema kwamba “*a person commits an offence of trafficking in person if that person: (a) recruits, transports, transfers, harbours, provides or receives a person by any means including those done under the pretext of domestic or overseas employment*”. Sasa tungependa kujua kwamba tunapokuwa kwa mfano, tunawachukua vijana wetu, tunawapa ajira ya majeshi, halafu tunawasafirisha kwenye nchi nyingine bila mkataba unaoeleweka na bila ruhusa ya Bunge, je, hiyo ni *abduction*? Halafu wanakwenda kule wanafanya kazi ya jeshi lakini pia malipo yao hayaeleweki!

Hii pia lazima iangaliwe kwamba pengine Serikali nayo inashiriki katika haya mambo ya *abduction* na mambo ya *trafficking* kwa sababu ukiangalia *experience* kutoka nyuma, kuna watu ambao walipotelea huko. Msumbiji kwa mfano, hawakulipwa fidia, familia zao hazikulipwa fidia, makaburi yao hayajulikani yalipo! Sasa hii inatokana na human *trafficking*. Kwa hiyo, suala la *trafficking* limekuwa ni la kutisha.

Pia ningependa Serikali iangalie kwamba je, wale ambao wanalazimika kupita katika nchi yetu kwa sababu katika nchi yao kuna matatizo, hiyo nayo inaitwa ni *trafficking*? Kwa sababu kama Watanzania wenyewe wako tayari kutoroka hapa nchini waende kwingine, kwa nini watu wakitoka kama Somalia au Ethiopia, wakipita hapa wanakamatwa wakiwa kwenye malori? Inaonekana labda ni *trafficking*. Na wale Watanzania wanaowasaidia kwa sababu mila kwa mfano za Afrika, mtu akikimbia kutoka eneo lingine kwa sababu ya tabu, akija kwako huruhusiwi kumtoa kwa adui yake au kumfukuza.

Mila na desturi zinataka umkaribishe, umpe chakula, umsindikize umwonyeshe njia na ndicho kilichosababisha kwa mfano sisi tunaokaa mipakani wanasema tunakaribisha Wasomali, kumbe ni mtu amekimbia amekuja kwako, sasa unaona huyu ni mwanadamu nitamsaidiaje. Haya unakamatwa pengine baadaye utashitakiwa kwa sababu ya *trafficking*. Hili nalo Serikali ilianganalie kwamba hawa watu ambao wanapita tu, wanawezaje kupewa *safe passage* kwa sababu nao ni wanadamu na wanatoka kule kwa sababu ya shida na kule wanakokwenda hawarudishwi kwa sababu wanakwenda Afrika Kusini kutafuta maisha, wanakwenda nchi nyingine. Kwa hiyo, nao pia wapewe *safe passage* maana ni wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningependa kuiomba Serikali yetu ianganalie suala la ajira kwa sababu vijana wengi ambao ndiyo asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania hawana ajira. Hii ni *inducement* au ni *cohesion* au *enticement* ambayo inawafanya wakubali hata kwenda nchi za nje kutumika kama watumwa wakati ambapo wangeweza kufanya kazi hapa nchini. Kwa mfano, kama mazingira ya vijijini yangeboreshwa watu wasingekuwa na hamu ya kutoka pale kwenda mijini. Pia tuanganalie

mji kama wa Dar es Salaam, inasemekana umejaa madanguro ya kila aina na watu wanatumikishwa pale. Kwa hiyo, hii sheria pia iangalie kwamba mtu anapohiari mwenyewe kutumikishwa, inatokana na nini? Pengine inatokana na shida na ile shida sasa ndiyo tuangalie namna ya kuitatua ili watu wasiwe wanaingizwa katika utumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache nashukuru kwa kuniruhusu. Nadhani Serikali itafanyia kazi, *message sent!* (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa orodha ya asubuhi hii, Mheshimiwa Chacha Wangwe ndiye alikuwa anamalizia. Kwa tafsiri ambazo anazihitaji, Mheshimiwa Waziri anahitaji muda kuzichambua ili *human trafficking* hii ieleweke vizuri zaidi. Nilipata ujumbe kidogo kutoka kwa Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Lembeli akikumbusha tu kwamba Taifa *Stars* itakuwa na mechi na Kenya na akawa anauliza anamwona Mheshimiwa Bendera humu ndani kwamba vipi maandalizi huko? Na mimi *message* nimekwishaifikisha, Mheshimiwa Bendera amekwishasikia! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, ili kutoa nafasi kwa Serikali kuweza kuchambua na kupata majibu ya kuweza kuwasilisha katika Bunge hili Tukufu, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni ambapo moja kwa moja tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri.

*(Saa 6.30 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu wa Mwaka 2008**  
***(The Anti-Trafficking in Persons Bill 2008)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kama mtakumbuka asubuhi wachangiaji wote walipata nafasi na kwa hiyo hatuna mchangiaji wa ziada, moja kwa moja namwita Mheshimiwa Naibu Waziri ili tuanze kupata majibu ya hoja tulizozitoa.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze kwa kuletwa Muswada huu wenye lengo la kukataza na kuadhibu usafirishaji haramu wa binadamu hasa wanawake na watoto. Kimsingi wanawake na watoto ni kundi muhimu sana katika jamii lakini pia ni kundi ambalo limesahaulika sana katika huduma mbalimbali na ndio maana tunaambiwa haki za wanawake, siku ya mwanamke na



tunaona kuna maazimio mengi sana ya kumlinda mwanamke nchini na duniani kote kama *Beijing Declaration* na ndio maana tunaongelea asilimia 50 – 50 kwani huwezi kutaja historia ya binadamu awaye yeyote bila kumtaja mwanamke. Hivyo, njia zote za unyanyapaa kwa mwanamke na watoto ni lazima zidhibitiwe ikiwa ni pamoja na kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *Section 7(2)(a)(b)*, tafsiri ipelekwe *Part I* ya Muswada ambayo inahusu tafsiri, *Part I, Section 3*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Section 19*, inazungumzia msaada na kuwalinda “*victims*”, waathirika wa *trafficking in human*. Muswada unamlenga Waziri, ni sawa lakini naona Waziri yuko mbali kama tatizo hili litakuwa limetokea Ludewa au Makete. Jambo hili lina wadau wengi sana kama vile mashirika ya dini, *NGOs*, ndugu na kadhalika, ni muhimu wadau hawa wakaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Section 19(3)* inaendelea kusema, Waziri atasaidia *subject to availability of resources*, hii ni *claw back clause*, utekelezaji wake unaweza kuwa mgumu. Napenda kuuliza je, Muswada huu umeandaa mafungu kwa ajili ya shughuli hizi? Maana Muswada huu unahitaji *centers for protection of victims*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba ni lazima Muswada huu utoe tafsiri ya neno *trafficking* ambalo halipo katika *interpretation*, labda kwa Kiswahili ni biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. *Part II* imeeleza *acts of Trafficking in persons* na sio *definition* ya *trafficking in persons*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu ni jambo dhahiri kabisa watu hupenda kwenda kwenye maeneo ambayo yana *income generation activities* za haraka, kwa mfano, Mufindi katika mashamba ya chai, *SAO HILL* na wapo wahusika ambao wana-*mobilize* vibarua na kadhalika, je, hii nayo ni *trafficking in human*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za majumbani (watoto) wa kazi, Muswada huu utakuwa ni wa msaada maana watoto watapata nafasi ya kusoma. Shukrani nyingi ziende Serikalini kwa kufuta ada maana itasaidia kutoa haki ya elimu kwa watoto wetu (*compulsory education*) ambapo Serikali imekuwa na *duty* ya kufuta ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unazuia usafirishaji haramu ambao wakati mwingine unaishia na *HIV, prostitution* na kadhalika lakini haujaangalia vyanzo/sababu za usafirishaji huu haramu kwamba ni kutokana na mahitaji ya *domestic – helpers* (wafanyakazi wa ndani) au ni nini? Naomba Serikali ilitafutie majibu kama mahitaji ni *Day-worker* katika madini/uvuvi basi watu wawe *trained* na waajiriwe kwa sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni moja ya njia za Serikali kulinda watu wake kama baba anavyolinda familia yake. Mwaka 2006/2007 Nchi kama Indonesia

mwaka ilikuwa na *statistics* kubwa sana za *trafficking in human*, walipoulizwa walisema hawana Sheria ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuwianisha usafirishaji haramu wa binadamu (*trafficking*) na tatizo la kiuchumi. *Trafficking as a problem of global economy, the need for cheap labour* kwa mfano Uingereza wanahitaji sana *cheap labour* kutoka nchi zinazoendelea lakini ni muhimu kumpa kipaumbele mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Section 32(m)*, iongezewe wajumbe maana wajumbe wote ni *intellectuals*, awepo na mzazi wa kawaida kutoka Serikali za Mitaa au mwananchi *preferable* mwanamke, hii itasaidia *participatory approach on trafficking the problem*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Lawrence Masha (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuwasilisha vizuri Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (*The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*). Ninaunga mkono Muswada huu.

Maoni yangu ni kwamba, kama Taifa, ili kuufanya Muswada na hatimaye Sheria hii iweze kufanya kazi, lazima tuangalie namna ya kuimarisha uchumi wetu ili kuondoa mwanya unaoruhusu usafirishaji haramu wa binadamu. Watu wetu wanasafirishwa kwa matumaini kuwa watapata maisha bora na hivyo kupata kazi, uchumi imara utatuondolea tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Wizara kwa kuandaa Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa muda huu ambao kumekuwepo na matatizo haya ya usafirishaji wa binadamu duniani pote. Angalizo ni kwamba kuna hizi mali ambazo zinapita bandari ya Dar es Salaam *on transit*, ni vizuri pia kama kutakuwepo na uwezekano wa kuzikagua kwa sababu vijana/watoto wengi wanasafirishwa kwa kutumia njia hii kutoka nchi moja mpaka nyingine.

Vilevile kuna wasichana wadogo wanasafirishwa kutoka vijijini kwa kuahidiwa kuwa watapelekwa mjini kupatiwa kazi na kulipwa mishahara mizuri lakini badala yake watoto hawa wanakwenda kuuzwa na wakishalipwa kwenye biashara hiyo, wanawarudishia wale matajiri wao zile fedha walizolipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Sheria hii inasemaje kuhusu vijana wanaofanya kazi katika migodi? Naomba hili neno *human trafficking* mtuelezee kwa mapana zaidi linaishia wapi?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi kwa Wizara na watendaji wote kwa kuuleta Muswada huu Bungeni. Hakika umeletwa kwa wakati kwa sababu ukubwa na upana wa tatizo hili sasa linaitingisha dunia. Tatizo hili ni utumwa mamboleo, linalingana na biashara ya silaha na madawa ya kulevya. Inasemekana faida inayopatikana kwa mwaka ni zaidi ya *USD* bilioni 30, wanawake na watoto ndio waathirika wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali izingatie sababu kubwa za matatizo haya, kwa mfano, utandawazi, umaskini, vita vya wenyewe kwa wenyewe, kukosa utawala bora pamoja matatizo ya jinsia. Serikali yetu iendelee na jitihada zake za kuboresha maisha ya wananchi wake na kuhakikisha kuwa mapato ya Taifa yanagawanywa kwa haki na kuacha kupeleka maendeleo sehemu moja tu ya Jamhuri yetu kuliko sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifahamu kwamba kuwashitaki na kuwapa kifungo hawa wahalifu hakutoshi, inatakiwa iandae mpango maalumu wa kuwakinga raia wake, kuwashitaki wahalifu wote na kuwalinda wahanga wote. Kwa sababu wahalifu hawa hutumia mbinu za udanganyifu mkubwa na hufanya shughuli zao kwa siri sana, basi Serikali lazima iwe *before* yaani itumie mbinu kubwa zaidi ili kupambana na wahalifu hawa. Naomba Serikali izingatie, kwa kuwa mara nyingi waathirika wa *human trafficking* huwa wanaadhibiwa kwa kuvunja Sheria ya Uhamiaji. Hili ni jambo baya, tutambue kuwa waathirika wa janga hili wanahitaji kuhurumiwa, kulindwa na kulipwa fidia. Aidha, Serikali iwaadhibu wahalifu hawa na ikiwezekana kuwafilisi mali zao.

Mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 ila naliomba Bunge likubali kuridhia mikataba yote ya kimataifa inayohusu biashara haramu ya *human trafficking*. Ahsante sana.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu ambao unahitajika sana nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kufafanua maana halisi ya Muswada huu. Kwa mfano, maana ya neno usafirishaji wa binadamu, je, usafirishaji huu ni wa ndani ya nchi au nje ya nchi? Kama tafsiri hii haielezwi kwa wananchi na wakaelewa, basi wale watu ambao wanaijua vema Sheria, wanaweza kuipotosha.

Katika Muswada huu, Kifungu cha 19, Serikali ina wajibu wa kuwalinda wananchi, kwa hiyo, uelewa wa Sheria hii ni muhimu. Ni wajibu pia wa wananchi kujilinda na kujizuia kusafirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasafirishwa kwa sababu maalumu na nyingi sana. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuangalia kwamba sababu nyingi kama si zote zinafahamika na kudhibitiwa. Sheria hii ni wokovu mkubwa kwa wanawake na watoto. Biashara hii huwaathiri sana wanawake ambao huongopewa na watu kuhamia mijini kwa

matumaini ya kupewa kazi ama kuolewa na hatimaye hawapati kazi wala elimu. Wale walioahidiwa kuolewa hawaolewi na huishia kuwa malaya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumezuka mtindo wa wageni kusafirisha wanawake kwa aina yake. Wanawake huolewa na mara moja mwanamke husafirishwa na mumewe kabla mwanamke huyo hajazaa. Wafikapo Ulaya huachwa lakini wakati huo wamekwishakuwa wananchi wa nchi zile ngeni, wamekuwa wageni lakini raia kwenye nchi ngeni. Kwa kuwa sisi Tanzania hatuna uraia wa nchi mbili, hivyo mwanamke huyo analazimika kuwa malaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Muswada umeletwa wakati muafaka na naunga mkono hoja hii.

Pili, nchini kwetu biashara hiyo haijashamiri sana isipokuwa mtindo au mbinu inayotumika ni uzamiaji. Mipango hufanywa kati ya wafanyabiashara walioko nje na mabaharia wanaokuwemo kwenye meli ambao huwashawishi vijana kwa kupatiwa kazi huko majuu.

Tatu, miaka ya hivi karibuni, vijana wengi wa kike na kiume wamekuwa wakienda nchi za kiarabu kwa wingi. Ni vema Serikali ikafuatilia hali hii hasa katika kujiridhisha kama safari hizo siyo mtindo wa biashara haramu ya binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri uwepo utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia mabango na vyombo vya habari, lengo liwe kuelezea athari zinazotokana na biashara hiyo haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe kunafanyika ukaguzi wa ghafla kwenye meli wakati zikiondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa pole kwa wachimbaji wadogo wa Mererani kwa vifo vilivyowapata. Pia natoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wote wa Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Lawrence Masha, (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, (Mb), kwa mara ya kwanza kuleta Muswada huu mara baada ya Rais kuwakabidhi Wizara hii. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo tayari tunaona matunda yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unalenga sana kuwasaidia wanawake na watoto. Biashara hii inawaathiri sana wanawake na watoto kwa ajili ya umaskini walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni yangu kama yafuatayo:-

(i) Ajira nchini iongezwe ili watu wasirubuniwe na kupelekwa nje kwa madai kuwa watapewa ajira;

(ii) Biashara hii haramu ifafanuliwe vizuri kwa wananchi, elimu itolewe ili watu wajue Sheria hii inawalenga watu gani;

(iii) Sheria hii itekelezwe haraka mara baada ya Rais kuweka saini; na

(iv) Sensa zifanyike vijijini ili tujue watu wangapi wamepelekwa nje ya nchi kwa biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na maoni ya Kamati na naomba Wizara iyazingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba Muswada huu upite bila kupingwa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu sana hasa kwa nchi yetu inayojali haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji haramu wa watu, nauona kwa mapana zaidi. Kuna wanaosafirishwa kutoka vijijini kwenda mijini kufanya kazi za ndani na waathirika zaidi ni wasichana wadogo, wapo pia vijana wafanyao kazi za ndani, wajulikanao kama *houseboy*. Vilevile wapo wasichana wanosafirishwa kwenda *Middle East* na nchi za Kiarabu kufanya kazi za ndani na wengine hupelekwa kuuza miili yao, wengine kwa mapenzi yao, wengine kwa kulazimishwa na aliyewasafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itoe tafsiri nzuri ya *human trafficking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iangalie kwa undani sababu za msingi zilizosababisha usafirishaji wa binadamu na wengi wao ni vijana na ni nguvu kazi ya Taifa kwa ujumla na hasa katika maeneo yao wanayatoka. Najua sababu kubwa ni uduni wa maisha ya vijijini na umaskini uliokithiri. Hivyo hii ni changamoto kwa Serikali kuboresha maisha ya wananchi hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muundo wa Kamati uzingatie jinsia na vilevile kuwepo Kamati ndogo ndogo katika ngazi za vijiji hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya kutosha kwa jamii inahitajika ili waelewe Muswada huu ambao punde utakuwa Sheria. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kuwa elimu itatolewa lakini nashauri ikiwezekana elimu itolewe kuanzia shule za msingi.

Hivyo Wizara iwasiliane/ishirikiane na Wizara ya Elimu ili uwepo uwezekano wa kuiweka kwenye mitaala ya elimu kama itakavyofanyika katika *issue* ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo, viongozi/wenyeviti wa vijiji na mitaa waelimishwe ili nao watoe elimu kwa njia ya mikutano ya hadhara katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iweke adhabu kali hasa kwa wale wanaosafirisha hao wanadamu kwa malengo yao tofauti. Nashauri kiwe kifungo cha miaka 30, adhabu hiyo itawapa woga wafanyao biashara hiyo haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri Sheria hii iwekwe kwenye lugha rahisi na kuwepo na vipindi vya radio. Muswada huo utakapokuwa Sheria uchapishwe kwenye magazeti ili wananchi wengi waweze kuifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwani imezingatia haki za binadamu, naomba ushauri wangu uzingatiwe. Pia naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana na ajira na ile Wizara inayoshughulikia masuala ya maendeleo ya jamii katika kuhakikisha tatizo hili linaisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nikiwa mkazi wa Lindi, niwape pole wenzetu wa Kilwa kwa ajali iliyotokea ya kuzama chombo chao majini na kupoteza maisha ya watu. Pia natoa pole kwa ajili ya mafuriko ya Mererani, Kyela na maafa yote nchini kama Waziri alivyosema wote kwa kweli inatugusa. Baada ya hapo, nimpongeze Waziri kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Mchango wangu kwa Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya binadamu ni haramu sana na kwa kweli ni udhalilishaji mkubwa kwa nchi ambayo mtu anayesafirishwa anatoka. Kwa hiyo, suala la kudhalilishwa nchi, ni aibu kubwa kwa mataifa ya nje. Sisi Tanzania tuliozoea amani na utulivu, ni aibu kwa tukio hilo, likomeshwe kabisa. Hili hakuna tofauti na utumwa, tunaweza kuita utumwa mamboleo. Kwa kuwa linafanana na linagusa utumwa, ni sawa na uvunjaji wa haki za binadamu. Kwa hiyo, napendekeza kuwepo kwa kipengele kinachoonyesha kuwa biashara ya binadamu ni sawa na biashara ya utumwa na ni sawa na utumwa mamboleo, kwa maana nyingine ni utumwa wa kisasa. Na hii ni uvunjaji wa haki za binadamu. Hapa naona hoja nzito inajitokeza ya neno utumwa mamboleo. Neno hilo liangaliwe kwa uzito wake na litafutiwe kifungu kwamba usafirishwaji haramu wa binadamu ni sawa na utumwa, kitu ambacho ni uvunjaji wa haki za binadamu.

**MHE. SUZAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji haramu wa binadamu, ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Usafirishwaji huu haramu ni sawa na utumwa. Katika dunia ya sasa, usafirishaji huu ni tishio kubwa na linagusa sehemu nyingi yaani ni *multi demensional threat*, ni tatizo la kiafya na pia linachochea ukuaji wa vitendo viovu yaani *organized crimes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji huu una madhara makubwa sana kwa waathirika wenyewe ambapo wanapata madhara kimaumbile (*physical*) pamoja na *emotional abuse*, vilevile kubakwa, wizi wa pasipoti na mara nyingine vifo. Lakini madhara ya usafirishaji huu yanaenda zaidi ya mtu binafsi, yanapunguza na kuhatarisha usalama wa mataifa yanayoguswa na uharamia huu. Wanaosafirishwa wako katika hatari kubwa na ni wale wasio na nguvu (*powerless minorities*) katika jamii, wengi wao ni wale wasiokuwa na makazi au wakimbizi wa vita *i.e. refugees*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na aina nyingi za uharamia huu ikiwa ni pamoja na watoto kwa kuwadanganya na kuwalaghai wazazi fedha kidogo kutokana na umaskini wao. Kundi lingine ni la wanawake ambao wanafikia asilimia 80 ya waathirika wote duniani. Wanawake hawa wako kwenye hatari ya kuingia katika biashara ya ngono (*sex trafficking*). Maharamia hutumia njia ya kulaghai kuwa watapata kazi nzuri na maisha mazuri lakini ukweli ni kuwa wanaishia kutaabika na kufanyiwa matendo ya kinyama na bila ujira.

Hivi karibuni kulikuwa na taarifa kuwa baadhi ya wasichana (Watanzania) huhifadhiwa Dar es Salaam na mama mmoja na baadaye hupelekewa Kongo na baadaye Ufaransa. Binti mmoja alitoroka na akaeleza yaliyomsibu. Sijui ni kwa jinsi gani Serikali imefuatilia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna bahati kwamba suala la usafirishaji si kubwa sana kama inavyoonekana lakini inawezekana kabisa idadi ikawa kubwa kwani hatuna *database* ya kujua nani yuko wapi na anafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nia ya usafirishaji huu haramu ni kwa wahusika (wasafirishaji) kujipatia fedha kwa kuuza watu, hali hii inapunguza sana uzalishaji katika nchi mbalimbali hususan Asia ambapo vijana wengi wamekwenda nchi za Magharibi na Marekani kwa lengo la kujitafutia riziki.

Hata wanapofika huko, kazi kubwa wanazofanya ni zile za chini kabisa kama *hotel attendant*, kudeki, kuuza *bar* na *clubs* na wengi wao huishia katika biashara za kuuza miili yao na hivyo kuhatarisha afya zao hasa ikizingatiwa janga la Ukimwi lililoikumba dunia. Wanaume nao hujikuta wakifanya kazi ngumu hivyo kupata madhara makubwa kiafya na hata kufariki.

Takwimu zinaonyesha kati ya watu 600,000 hadi 820,000 husafirishwa kila mwaka kupitia mipaka ya kimataifa na wengi wao huwa ni wanawake wanaoingia katika biashara ya ngono (*sex trade*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa za biashara hii haramu ni:-

- (i) Ukosefu wa fursa za ajira;
- (ii) Uwepo wa makundi maovu yaliyokuwa *organized*;

- (iii) Tofauti za maendeleo kimaeneo (*regional imbalances*);
- (iv) Uchumi usiolingana (*economic disparities*);
- (v) Ubaguzi katika jamii;
- (vi) Ufisadi katika Serikali;
- (vii) Kuyumba kisiasa (*political instability*);
- (viii) Mchafuko – vita;
- (ix) Kuhamisha wakazi kwa misingi ya kuleta miradi mikubwa bila uwepo wa taratibu nzuri za makazi mapya na mafao yao – Tabata case;
- (x) Kukua kwa kuwanyima haki na kutokujali maskini katika jamii;
- (xi) Kutokuwepo kwa adhabu kubwa kwa maharamia hawa yaani *traffickers*; na
- (xii) Mahitaji ya malaya (*prostitutes*) yako juu sana pamoja na aina ya kazi katika nchi zinazopokea, (*host*) *countries*. Hivyo, biashara hii ina faida kubwa sana na hivyo wasafirishaji wanaongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madhara yanayotokana na usafirishaji huu, inabidi Serikali ifanye mikakati ya wazi kuhakikisha kuwa wananchi wake hawauzwi nje ya nchi na hii itafanikiwa kwa kuhakikisha sababu za usafirishwaji huo nilizozitaja hazitokei hapa nchini. Lakini pia Serikali itoe hamasa kwa wananchi kwa kuwaeleza madhara ya usafirishwaji nchi za nje. Tumeona ni jinsi gani vijana wetu wanavyoteswa na wengine kutoswa majini na hata kuuawa wanapofika huko walikopelekwa. Lakini pia Serikali inapaswa kutoa elimu kwa polisi, *social welfare staff* na maafisa uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania pia ni lazima vituo vya watoto hasa yatima viangaliwe kwa makini kwa sababu wanaweza kuchukuliwa kwenda nchi nyingine kama ilivyotokea kule Chadi mwaka jana. Ni lazima wawekewe ulinzi wa kutosha. Lakini hata watoto wa mitaani nao wawekewe utaratibu ili wasichukuliwe nje au ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni la wasichana wa kazi (*house girls*). Kwa miaka mingi watoto wa kike hasa kutoka Mikoa ya Iringa na Singida, huletwa mijini kama *house girls* lakini baadaye hunyimwa mishahara na hivyo huingia au hupelekwa katika shughuli nyingine kama *commercial sex* na kuuza *bars*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ajira kwa watoto kama wale wa machimboni, ni usafirishwaji haramu na unyonyaji kwani watoto hawa hawalipwi ujira wa kutosha lakini kimataifa na kitaifa ajira kwa watoto ni *illegal* (ukiukwaji wa sheria). Ni matumaini



yangu kuwa Serikali itasimamia vizuri suala hili ili kupunguza tatizo la usafirishwaji haramu wa watu hususan kwa kulinda vizuri mipaka lakini pia kitengo cha uhamiaji kuwa makini katika kutoa pasipoti na wale wanaofanya biashara hiyo wapewe adhabu kali.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakupongeza wewe kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uzuri na kasi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ni nzuri na naomba Serikali iipitishwe na isimamie vema kwa maslahi ya wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua kali mno ichukuliwe kwa wakiukwaji wa Sheria hii na Watanzania wafahamishwe wahalifu wa ndani ya nchi na nje ya nchi kwa usafirishaji haramu wa binadamu. Wahalifu watangazwe na adhabu waliyopewa itambulike kwa Watanzania na ulimwengu pia ziendane na kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Sheria hii imechelewa sana kutokana na tabia ya usafirishaji binadamu kwenda kufanya kazi ambazo hazifanani na binadamu ndani ya nchi na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji haramu wa binadamu hasa ya wanawake na vijana, hupewa kazi za shuruba, hutumikishwa mithili ya ng'ombe wanaokokota jembe la mkono. Watoto wa kike hufanyiwa vitendo vya ngono bila ridhaa yao na hata kama akiridhia basi atafanyiwa kinyume mithili ya mwanamke aliyebakwa na zaidi ya watu wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe ili Sheria ieleweke, kwa kutotolewa elimu, wale tunaowaagiza wanaweza wakitumia vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafsi hii ili kuweza kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge leo asubuhi wakati tulipoweka muswada wetu kuhusu Biashara Haramu ya Binadamu wa Mwaka 2008 (*Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa ruhusa yako kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu hili. (*Makofi*)

Kwa kuwa Mheshimiwa Job Ndugai umechaguliwa bila ya kuwa na mpinzani na umepata kura za Wabunge wote waliokuwa katika kikao, hii inadhihirisha kabisa imani kubwa waliyonayo Wabunge kwako wewe kwa utendaji kazi wako na kwa umahiri wako katika kuendesha shughuli za Bunge, kwa hiyo, naomba nikupongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nichukue fursa hii niwapongeze Wenyeviti wawili waliochaguliwa pamoja nawe, Mheshimiwa Jenister Mhagama na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid. Baada ya kusema hayo ningependa nichukue nafasi hii kumtakia Spika wa Bunge letu, Naibu Spika na Wabunge wote, mema katika Mkutano wetu wa Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii adhimu niseme kwamba leo wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa akielezea juu ya muswada huu, alizungumzia kwa ujumla juu ya majonzi tuliyokuwa nayo kama Wizara na alitoa pole mbalimbali kwa misiba iliyotokea hapa nchini. Kwa hiyo, nisingependa kurudia hilo isipokuwa ningependa tu kusema kwamba tunatoa pole zetu na tunapeleka mkono wa tanzia kwa jamaa wote ambao kwa njia moja au nyingine wameguswa na matukio ambayo yametokana na vifo ambavyo vimetokea katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunitewa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hapo hapo nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ameonyesha kabisa moyo wa kutupokea na kutufunza katika shughuli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii nimshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa kazi ambayo naona tumeianza vizuri na naona ana imani kubwa kwangu mimi na ningependa niseme hadharani kwamba nashukuru kwa imani kubwa aliyonayo kwangu katika utendaji wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nachukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura ambao ndiyo waajiri wangu kwani wao ndiyo walionichagua na kunipigia kura na hatimaye kuniwezesha kuja Bungeni na wameweka imani yao kwangu niweze kuwasemea na kuwatetea. Ningeomba nichukue nafasi hii niwashukuru kwa imani kubwa waliyonayo kwangu mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kuhusu muswada ambao tunao mbele yetu unaohusu Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (*Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*), kwa kweli binafsi nasema tumefarijika asubuhi ya leo na nimefurahi sana kwa maoni mbalimbali ambayo tumeyapata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Mapendekezo ambayo wametupa na mawazo waliyoyatoa na kwa uhakika tumejitahidi kadri ya uwezo wetu kuyazingatia kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa katika kuanza kuyatazama mapendekezo na baadhi ya maoni ambayo yametolewa asubuhi ya leo, naomba nitazame baadhi ya mapendekezo ambayo yametolewa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiwa Dar es Salaam tulishirikiana kikamilifu na Kamati ya Bunge na walitoa maoni mazuri ambayo yaliboresha muswada na tuliyapokea na kuyazingatia. Ningependa nichukue fursa hii nitaje marekebisho katika baadhi ya vifungu vya miswada ambayo yalitolewa na Kamati na hata leo yamerejewa katika hotuba iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Maoni yote yamezingatiwa kama yalivyowasilishwa kwenye Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*) lililowasilishwa ambalo mtalipata wakati wa Kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawazo na mapendekezo ambayo yametoka Kambi ya Upinzani, ningependa nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu kwa niaba ya Kamati yake kwa mapendekezo na mawazo mazuri ambayo wameyatoa asubuhi ya leo.

Niseme kwamba mengi tumeyapokea na tumeyazingatia. Kwa mfano, wakati akitoa hotuba yake amezungumzia juu ya kifungu cha 5(5) kinachohusu kiwango cha adhabu chini ya kifungu hicho kwa aliyetenda kosa chini ya kifungu cha 4 kulingana na uharibifu na sisi tunamjibu kwa kusema kwamba kiwango cha adhabu kimezingatiwa chini ya vifungu 5(3) 6(4), 7(3) na kifungu cha 8, kiwango hicho ni kikubwa cha kutosha kulingana na aina ya kosa. Vifungu hivi vinawapa mamlaka ya kutosha mahakimu na majaji.

Lakini hapo hapo Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani wametoa rai yao wakati walipokuwa wakijaribu kuzungumzia juu ya kifungu cha 18(2) kuwa kiongezwe neno *qualified* ili isomeke *qualified social welfare offices*. Tumetazama ushauri huu, hauna tatizo lakini tunasema kwamba Serikali wakati ikiwa inaajiri watu kwa kawaida inapotangaza hizi nafasi ni nafasi ambazo tunaeleza kwamba wanatakiwa watu wa vigezo vya aina fulani na uzoefu wa aina fulani na kisomo cha aina fulani, kwa hiyo, hali ya *qualification* ya wale ambao wanahitajika inakuwa imezingatiwa, hata hivyo ni ushauri mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 ambacho wameshauri kuweka albaki ya faini baada ya kulipa faini baada ya kulipwa fidia kwa waathirika kama chanzo cha mapato kwa ajili ya mfuko, tunasema kwamba ushauri huu unakubalika na utazingatiwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mawazo mbalimbali kama nilivyosema, tumepata mawazo ya maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Suzan Lyimo, ambaye alitamka kwamba hivi karibuni katika maandishi yake, kulikuwa na taarifa kuwa baadhi ya wasichana wa Kitanzania kutoka Dar es Salaam kusafirishwa kwenda Ufaransa kupitia *Democratic Republic of Congo (DRC)* na akauliza kama Serikali ina taarifa juu ya hilo na inalifuatilia kwa kiasi gani. Jibu letu ni kwamba Serikali inayo taarifa, Idara ya Polisi kupitia Kitengo chake cha Upelelezi sehemu inayoshughulikia makosa dhidi ya binadamu ambacho hushughulikia *Anti-Trafficking in Persons* inafuatilia kwa karibu na inazo taarifa nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitishwa kwa sheria hii kutasaidia kuyashughulikia masuala haya kikamilifu. Mheshimiwa Lyimo pia ameuliza kama Serikali ina *data base* ya kujua nani yupo wapi na anafanya nini. Tunasema kweli hiyo *data base* hatuna na haijakuwepo, lakini tukipitisha sheria hii tutajitahidi tuwe na hiyo *data base* lakini naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba haya ni mambo ambayo yanahitaji fedha katika utekelezaji, nia na shabaha ni nzuri lakini utekelezaji wake utategemea sana na jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha ili tuweze kutimiza azma yetu hiyo.

Mheshimiwa Suzan Lyimo katika mchango wake pia aliweza kuainisha sababu za kuwepo kwa biashara hii haramu na ameishauri Serikali kuweka mikakati ya wazi ya kupambana na biashara hii haramu. Serikali inayo mikakati ya kudhibiti tatizo hili, kinachosubiriwa ni sheria hii kupitishwa ili kasi iongezeke zaidi, hata hivyo, hatua mbalimbali zinachukuliwa kwa yale makosa yanayoambatana na kosa hili, kwa mfano, masuala ya kubaka.

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni yeye ametoa rai yake akitaka Serikali itoe elimu ya kutosha kwa Umma na ametaka sheria iwekwe bayana kwa lugha ya Kiswahili. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis kwamba huu ni mmoja wa mikakati muhimu wa Serikali ili wananchi waweze kufahamu madhara ya biashara hii haramu hatimaye watoe ushirikiano katika udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na nasaha na ushauri mbalimbali kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe. Yeye anasema biashara hii haijashamiri sana hapa nchini na kwa kiasi kikubwa inafanywa kupitia uzamiaji ambao ni kati ya wafanyabiashara hiyo na mabaharia wa meli kwa kishawishi na ulaghai kwamba watawapatia kazi huko nje, hivyo Serikali iwe inafanya ukaguzi wa ghafla katika meli zinaposafiri kwenda nje. Ushauri huu ni mzuri na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba utazingatiwa. Pia ameshauri kwamba miaka ya hivi karibuni vijana wengi wa kiume na wa kike wamekuwa wakienda nchi za kiarabu, ni vema Serikali ikajiridhisha kama safari hizo siyo za biashara haramu za usafirishaji wa binadamu. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ushauri huo utazingatiwa.

Mheshimiwa Fatma Mikidadi yeye katika rai yake amesema kwamba hii ni biashara haramu ambayo ni sawa na utumwa mambo leo kwani inadhalilisha nchi yetu na ni uvunjaji wa haki za binadamu, kiwekwe kifungu katika muswada huu ambacho kinasema usafirishaji haramu wa binadamu ni sawa na utumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezingatia mawazo ya Mheshimiwa Fatma Mikidadi na kwa kifupi biashara hii haramu maana yake nyingine ni utumwa wa kisasa, ni mbinu tu ndizo zimebadilika na hilo tumelizingatia.

Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtullya, amesema kwamba tatizo hili ni sawa na utumwa mambo leo ambalo linataka kulingana na biashara ya silaha na madawa ya kulevya na waathirika wakubwa ni wanawake na watoto, ni vema sasa Serikali ikazingatia sababu kubwa za matatizo haya. Hilo tunakubaliana nalo na tunasema tatizo hili ni sawa na biashara haramu ya silaha na madawa ya kulevya. Makosa hayo yote

matatu yapo kwenye kundi moja linaloitwa biashara ya magenge ya kihalifu yanayovuka mipaka (*trans-national organised crime*). Wanaofanya biashara hii wanasema kwamba hii ni biashara salama kuliko ya madawa ya kulevya na ya silaha na ni ya tatu kwa faida baada ya silaha na madawa ya kulevya. Ningeomba Bunge lielewe kwamba hili tatizo ni kubwa, waelewe kwamba huu ni mkakati mkubwa kwa sababu watu ambao wapo katika shughuli hii na takwimu zinaonesha kwamba biashara hii inashamiri sana kwa sababu walio ndani ya biashara hii wanaamini kabisa ni biashara ambayo kidogo ni tulivu na ina usalama kuliko biashara ya madawa ya kulevya na biashara ya silaha.

Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum yeye ameomba kujua ni mikakati gani Serikali iliyonayo kuhusu elimu itakayotolewa kwa wananchi. Hili litakuwa ni jukumu moja kubwa katika mikakati muhimu na tayari tumejiandaa na imekwishaanza.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha alikuwa anataka kujua maudhui ya sheria hii. Kwa maneno machache maudhui ya sheria ni kudhibiti biashara ya binadamu ndani na nje ya nchi. Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezungumzia juu ya uchumi duni na kuwa chanzo cha biashara hii. Hii ni kweli lakini pia ziko nchi ambazo uchumi wao ni mzuri lakini pia biashara hii inafanyika lakini sababu tunatofautiana nchi kwa nchi na biashara kubwa duniani lakini tunasema kwamba tutadhibiti biashara hii. Na Serikali itajitahidi kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaimarika na hiyo itasaidia katika kuzuia vijana wetu au watu wengine ambao wanaweza wakakumbwa na biashara haramu.

Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhanywa, Mbunge wa Viti Maalum, ameshauri tafsiri itolewe na tunamwambia kwamba limezingatiwa. Pia amezungumzia juu ya muundo wa Kamati uzingatie uwiano na jinsia, hili limezingatiwa. Vilevile anataka elimu ya kutosha itolewe na tunasema kwamba hilo nalo limezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tumemsikia Mheshimiwa Lediana Mng'ongo ambaye amezungumza kwa machungu sana kuhusu suala hili na ametoa ushauri jinsi Serikali inavyoweza kukabiliana na tatizo hili sheria itakapopitishwa. Amezungumza kwamba muswada utafsiriwe katika Kiswahili, hili nimekwishasema kwamba hiyo ni azma ya Serikali ambapo muswada utakapopitishwa kuwa sheria basi sheria hiyo itatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

Pia ameshauri kwamba utafiti kuhusu sababu za biashara hii ufanyike, amesema umuhimu wa utafiti huu ni mkubwa na tunakubaliana naye, Wizara itatekeleza kulingana na uwezo wake wa kifedha, maana yake tatizo kwa kweli ni kubwa lakini hatuwezi tukasema kila kitu kifanyike kwa wakati mmoja. Jambo la muhimu ni kuwa na sheria halafu mengine tutayatekeleza awamu kwa awamu kutokana na nguvu ambayo tunakuwa nayo katika wakati huo. Vilevile ametaka kujua je, nchi zinazotuzunguka wanazo sheria kama hii, kwa kweli mpaka sasa ni nchi ya Malawi ambayo ina sheria kama yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama naye alitaka kujua kama hii sheria itawekwa katika lugha ya Kiswahili. Jibu letu ni kwamba ikishapitishwa tutafanya hivyo na ndiyo azma ya Serikali. Pia amezungumzia juu ya Kamati zianzie ngazi ya Wilaya, hili ni sahihi na linazingatiwa. Hali kadhalika amezungumzia juu ya hali ngumu ya maisha, ni mojawapo ya chanzo cha kujiingiza katika biashara ya *trafficking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu jingine ambalo linahusiana na wazo kama hili, ni sawa Serikali itachukua hatua mbalimbali za kuimarisha uchumi. Lakini ningeomba Waheshimiwa Wabunge muelewe kwamba nimesema biashara hii hata katika mataifa makubwa ndani kwa ndani wao ipo wakati uchumi wao ni mzuri. Sina haja ya kutaja ni nchi gani lakini hata nchi ambayo ni kubwa kuliko zote na ina nguvu kuliko zote duniani hii biashara ipo na kila mwaka wanatoa ripoti na ripoti yao inakwenda katika Bunge lao ikieleza ni jitihada gani zinafanyika katika kupambana na tatizo hili. Kwa hiyo, nchi za *South East Asia* zinakwenda vizuri kiuchumi lakini tatizo hili lipo, nchi za *Latin America* zinakwenda vizuri kiuchumi kuliko sisi lakini tatizo hili lipo, ni tatizo la kilimwengu lakini sisi tuta-*play part* yetu na tutahakikisha kwamba tunafanya yale ambayo tunaweza kufanya kuhakikisha kwamba biashara hii haishamiri na haiendelee katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Haji Sereweji, tumeyapokea mawazo yake na kuyazingatia. Amezungumzia kwamba elimu itolewe kuhusu jambo hili na amewekea mkazo kwamba lazima Watanzania waelewe ukubwa wa jambo hili, tumelizingatia. Na amezungumzia kwamba Kamati izingatie watu wenye wadhifa wa juu, hili nataka kumhakikishia kwamba litaangaliwa na atapata jibu kuhusu suala hili na kuna wazo la kusema kuwa hili jambo liende hadi ngazi za Wilaya, hii ni sahihi na imezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Muswada huu mawazo yaliyojitokeza asubuhi ya leo yalikuwa hayajapishana sana, na mengi yalieleza ukubwa wa tatizo lakini pia uchungu wa tatizo na mengi yalieleza ni vipi vijana wengi wameathirika na akina mama wengi walikuwa wanahusika zaidi. Na tunasema kwa kweli tumezingatia na mawazo mazuri tumeyapokea na sasa iliyobaki ni sisi kuyafanyia kazi, muswada huu ukishapitishwa na Rais atakaporidhia litakalofuatwa ni sisi kuhakikisha kwamba sheria hii inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya, machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, moja kwa moja naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Laurance Masha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa

maandishi, naomba kwa idhini yako niwatambue Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Kwerekwe, Mheshimiwa Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Chacha Wangwe Mbunge wa Tarime, na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulya, Mbunge wa Rufuji, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamis, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha na Mheshimiwa Mhonga Ruhanywa, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Ulinzi na Usalama, Kambi ya Upinzani pamoja na wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi kwa kuunga mkono muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naahidi kwamba Serikali itafanyia kazi michango na mawazo mazuri yaliyotolewa na wote. Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Naibu Waziri kwa kunisaidia kujibu hoja nyingi zilizotolewa na wabunge kwa ufanisi na umakini, naomba sasa kwa idhini yako nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kwa kuelezea kwa undani maudhui ya Muswada wa sheria hii ambao uko mbele yetu siku ya leo. Muswada huu ni wa Sheria ya kuzuia Biashara haramu ya usafirishaji nje na ndani ya nchi hasa ya watoto, wanawake na vijana. Una maeneo makuu manne, na maeneo haya ni kuwapata, kuwasafirisha, kuwahifadhi na kuwatumikisha waathirika hao katika hii biashara haramu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia haya maeneo makuu manne kwa sababu ni lazima izingatiwe kwamba maeneo hayo manne ni lazima yachukuliwe kwa pamoja...! Samahani nakumbushwa kwamba kulikuwa na Mbunge mwingine Mheshimiwa Lucy Owenya, naye alichangia kwa maandishi, samahani sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema kwamba haya maeneo makuu manne kuwapata, kuwasafirisha, kuwahifadhi na kuwatumikisha waathirika hao ni lazima

yapatikane kwa pamoja, ni kuyachukulia haya maeneo kwa pamoja ndiyo tunapata kosa la kusafirisha binadamu ambalo ndilo tunaliongelea siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuisitiza hilo kwa sababu kuna watu ambao wameongelea suala la vijana ambao wanaondoka Tanzania kwenda kufanya kazi nje. Mtu kwenda kutafuta maisha bora nje ya Tanzania kama hivi vigezo vinne nilivyoviongelea havipo haichukuliwi kwamba kulikuwa na biashara haramu ya kusafirisha nje au ndani ya nchi. Kuna biashara haramu ya kusafirisha binadamu nje au ndani ya nchi, pia pale ambapo tunaongelea suala la kusafirisha binadamu ndani ya nchi, hili suala la kusafirisha wafanyakazi wa ndani (*servants*) hawaingii ndani ya Sheria hii mpaka pale ambapo inadhihirika kwamba hawa watu, moja, hawana uhuru pale walipo, pili, hawalipwi mshahara kutokana na sheria zetu za Tanzania. Tatu, kuna ukiukwaji wa sheria zetu kuhusu umri na masuala mengine kama hayo katika ajira yao.

Suala la kusema tu kwamba mtu amechukuliwa kutoka Iringa au Mwanza au sehemu nyingine ya nchi na amekuwa mfanyakazi wa ndani haina mantiki kwamba huyu mtu amesafirishwa kwa tafsiri ya Sheria yetu hii. Sasa ningependa hilo lieleweke, vile vipengele vinne ambavyo nimeviongelea lazima viwepo, kuwapata, kuwasafirisha, kuwahifadhi na nikisema kuwahifadhi, tukiongelea kwa mfano, *domestic servants* maana yake ni kwamba umewaweka katika hali ambapo hawawezi kuondoka wenyewe.

Kwa hiyo, ina maana kwamba kama una mfanyakazi wako wa ndani ya nyumba ambaye anaruhusiwa wikiendi kwenda Kanisani, ina maana kwamba angetaka kutoroka angeweza kutoroka, hapo huwezi kuhesabika kwamba umefanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu. Hivi vipengele vinne vyote vinatakiwa kuwepo.

Nilisema kwamba nilieleze hilo kwa uwazi kwa sababu tumeongelea hapa watu wa *green pastures*, imeongelewa wafanyakazi wa jeshi wanaopelekwa nje, hawa ni watu ambao wanafanya kazi kwa hiari yao. Wanalipwa mshahara unaotakiwa, hawa kwa kweli hawawezi kuingizwa katika biashara haramu ya kusafirisha binadamu. Ndugu yangu ambaye aliongelea wanafunzi ambao wanalima kwenye mashamba ya watu ningependa kusema wazi kwa tafsiri niliyoeleza hapa kwa siku ya leo na hao hawaingii katika biashara ya kusafirisha binadamu kama ilivyoelezwa ndani ya Sheria yetu hii leo. (*Makofi*)

Kuna Wabunge ambao wameongelea suala la muundo wa Kamati. Kuna wale ambao wamesema kwamba huu muundo wa Kamati mbona tunataja vyeo. Ningependa kusema kwamba Kamati hii ambayo tunaiongelea ni Kamati ya Kitaaluma. Tunahitaji watu ambao wana taaluma maalumu ambao wangeweza kusaidia kuishauri Serikali kwa kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi namna ya kudhibiti suala la usafirishaji wa binadamu haramu kama ilivyozingatiwa ndani ya Sheria yetu. Limeongelewa suala la kuwachukua wastaafu. Naomba nieleze kwamba chini ya Kifungu cha 31 baada ya marekebisho haiongelewi wastaafu peke yao, tunaongelea wastaafu pamoja na wale ambao wako kazini.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kuwa kuna watu ambao wamestaafu ambao hawajachoka, tumeongelea suala la watu ambao wamechoka, nafikiri angetuwa hapa Mheshimiwa Spika, ambaye kwa kweli amekwishafikia umri wa kustaafu na anafanya kazi kwa *standard and speed* asingekubali kwamba yeye kachoka na asingeweza kuteuliwa katika nafasi kama hii.

Naomba Waheshimiwa Wabunge wazingatie kwamba Waziri katika kutekeleza jukumu lake atahakikisha kwamba hatateua watu ambao wamechoka na atateua watu ambao wana uwezo wa kufanya kazi ambayo inategemewa kufanywa chini ya Sheria yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo imetolewa kuhusu kuingiza akina mama ndani ya Kamati. Katika *Schedule Amendments* ya pili ambayo imetolewa ndani ya Bunge hivi punde mtaona kwamba tumekubali wazo hilo na chini ya marekebisho ambayo tumeleta mbele yenu tumesema kwamba idadi ya akina mama ambayo watateuliwa kwenye Kamati hii wasipungue theluthi moja ya Kamati, kwa hiyo, hilo tumezingatia na watakuwepo ndani ya Kamati.

Suala la Kamati hii kufika mpaka ngazi ya Wilaya, ningependa kukufahamisha kwamba tayari hivi sasa tunavyoongea tunavyo vikosi kazi ambavyo vinafanya kazi hii kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kamati ambayo tumeongelea hivi sasa ni Kamati kwenye ngazi ya Taifa, na hizi Kamati zitaendelea kufanya kazi, tutaendelea kushirikiana nao ili kuwapata wale watu ambao wanafanya biashara ya kusafirisha binadamu.

Ningependa tu kusema kwamba kulikuwa na wazo kwamba tafsiri ambazo zinaonekana chini ya kifungu cha nne zingerudi katika eneo katika kifungu cha tatu. Napenda kujibu kwamba katika kuandika Sheria kuna namna nyingi za kuweza kuingiza masuala ya tafsiri kwenye Sheria na kutokana na upana wa wigo ambao tulikuwa tunajaribu kuingiza katika kuelezea neno *trafficking* ni nini, ilionekana vema kwamba hii ionekane pale katika eneo la kifungu cha nne badala ya kuingiza katika kifungu cha tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni suala la *legislative drafting* na haina maana kwamba tafsiri ambazo zimewekwa pale hazina uzito kama tafisi ambazo zimeingizwa katika kifungu cha tatu. Lazima nieleze kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameongelea hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa umakini na karibu hoja zote alikuwa amekwishazipitia. Niliona kwamba mimi nje nisimame hapa mbele yenu niwaeleze maudhui na nipitie yale ambayo mwenzangu alikuwa hajayaongelea. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge muupitiche Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu kwa hatua inayofuata!

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

#### **Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008)**

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 35  
Ibara ya 36  
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 39  
Ibara ya 40  
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa  
Mwaka 2008 (*The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (*The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*) ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa kadri ya taratibu za Bunge tumefikia mwisho wa shughuli ya Muswada huu. Hatua iliyobakia ni ya kupeleka mbele ya Mheshimiwa Rais ili aweze kuubariki ukamilike kuwa Sheria kamili. Nina tangazo moja kutoka kwa Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye anawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote kushiriki katika hafla ya uzinduzi wa matembezi ya hisani kwa ajili ya kuchangia chakula cha watoto wa shule za msingi.

Matembezi hayo yameratibiwa na *United Nations World Food Programme* na yatafanyika tarehe 12 Aprili, 2008 Viwanja vya *Nyerere Square* saa 3.30 asubuhi katikati ya Mji wetu wa Dodoma. Narudia, Mheshimiwa Mkuu wa Dodoma anatalika Waheshimiwa Wabunge wote tarehe 12 kesho pale Viwanja vya *Nyerere Square*, saa 3.30 asubuhi kwa ajili ya uzinduzi wa matembezi ya hisani kuchangia chakula cha watoto wa shule za msingi.

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya tangazo hilo shughuli zilizokuwa zimepangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika. Naomba kuchukua fursa hii kuliahirisha Bunge hadi Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.38 Jioni Bunge Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 14 Aprili, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*